**Askofu** Pengo atoa angalizo uendeshaji wa Bandari

UKURASA 3



**Mwanafunzi** wa UDOM alimtumia ujumbe mama kabla ya kuuawa

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Juni 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581346

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


## UPANDIKIZAJI UUME

# 40,000 wasaka elimu Hospitali ya Mkapa

• **Madaktari** bingwa wafafanua ufanisi, wasema ni suluhisho wenye shida ya nguvu za kiume...*Ukurasa 2*



Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) walipopandikiza uume kwa wahitaji wawili hospitalini hapo Jumatano ya wiki iliyopita. Ni upandikizaji wa kwanza kufanywa nchini. **PICHA: BMH**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MAJALIWA: SERIKALI IMESIKIA KILIO KODI TAULO ZA KIKE



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imesikia kilio cha wadau kuhusu kuwapo...



UKURASA WA 5

### CHONGOLO ALIA NA MILA KANDAMIZI KWA JAMII

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ame...

UKURASA WA 19

### RC, POLISI WAVAMIA HARUSI NA KUTIBUA NDOA YA MWANAFUNZI

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akiwa na wadau wa msaada wa kisheria pamoja na Jeshi la Polisi...

## Mbowe aenda Uingereza na hoja nyeti ya kidemokrasia

UKURASA 3



UKURASA 2

# Hoja 10 kutikisa mjadala bajeti ya serikali 2023/24

**MICHEZO** **MAYELE AOMBA KUONDOKA YANGA** UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

UPANDIKIZAJI UUME

# 40,000 wasaka elimu Hospitali ya Mkapa

**Na Christina Mwakangale**

SIKU chache baada ya wanaume wawili kupandikizwa uume katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) mkoani Dodoma, takriban watu 40,000 wamewasiliana na uongozi wa hospitali hiyo na wengine kufika hospitalini wakitaka kufahamu namna ya kupata huduma hiyo.

Vilevile, uongozi wa hospitali hiyo umesema wanaume wawili waliofanyiwa upandikizaji uliochukua saa mbili kwa kila mmoja, watatakiwa kuwa chini ya uangalizi kwa kuhudhuria kliniki, huku wakitakiwa kufuata sharti la kukaa bila kushiriki tendo la ndoa kwa wiki sita.

Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Mkojo wa hospitali hiyo, Dk. Remigius Rugakingira, katika mazungumzo na Nipashe jana kuhusu huduma hiyo na masharti kwa waliopandikizwa, alitaja idadi hiyo ya watu wanaohitaji kufahamu kuhusu huduma hiyo. Wapo waliofika hospitalini na waliowasiliana na uongozi kwa njia ya mtandao.

Alisema wanaume wawili hao walipandikizwa uume kutokana na kushindwa kushiriki tendo la ndoa, hivyo kuwa sababu ya kushindwa kutungisha mimba na hata kuishi kwa msongo wa mawazo. "Mgonjwa tunalazimika tunamfanyie mapitio kila mara. Huu ni upandikizaji wa kwanza. Ili kujua maendeleo ya wagonjwa hawa, tutaendelea kuwafuatilia.

"Huduma hii mpya ya kuwezesha uume kusimamia tena tumeshirikiana na wenzetu kutoka Ufaransa. Tumebaini wengi wana tatizo na elimu ni duni. Huduma hii ni suluhisho kwa nguvu za kiume," alisema Dk. Rugakingira.

Juni 14, mwaka huu, wanaume wawili waliokuwa na tatizo la nguvu za kiume kutokana na matatizo mbalimbali ya kiafya, walifanyiwa upasuaji na kuwekewa vipandikizi hospitalini huko.

Upandikizaji huo ulifanywa kwa ushirikiano kati ya Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa Mfumo wa Mkojo nchini (TAUS) na Daktari Bingwa wa Mfumo wa Mkojo kutoka Ufaransa. Dk. Rugakingira aliutaja ni huduma ya matibabu iliyotolewa kwa mara ya kwanza nchini. Alisema Hospitali ya Benjamin Mkapa inajali afya ya wanaume na upasuaji kama huo unaweza kufanyika Tanzania.

Dk. Liuba Nyamsogolo, kiongozi wa TAUS, alisema wamefikia hatua hiyo kutokana na kuwapo watu wengi wenye matatizo ya nguvu za kiume nchini na Afrika kwa ujumla.

"Mojawapo ya madhumuni ya TAUS ni kuendeleza wataalamu nchini kwa kushirikiana ma wataalamu kutoka nje ili kuleta nchini teknolojia inayopatikana duniani na kutibu magonjwa kama haya kwa wale wenye matatizo," alisema Dk. Nyamsogolo.

Msemaji wa BMH, Jeremiah Mbwambo, alielezea huduma hiyo, akitamka: "Hospitali ya Benjamin Mkapa imekuwa Hospitali ya kwanza nchini kufanya upasuaji wa kuweka vipandikizi kwenye uume kwa wagonjwa wenye matatizo ya nguvu za kiume.

"Serikali ya awamu ya sita imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kuiwezesha teknolojia za kisasa za matibabu ili kuwapatia matibabu thabiti wananchi."


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
19.06.2023

TAARIFA KWA UMMA


1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **23.06.2023 hadi 07.07.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha gari tupu wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili:

**NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - Mita 36.5**
   **Upana - Mita 7.20**
   **Kimo - Mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro** mpaka **Mlandizi**, magari yatasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri).*** Kutoka **Mlandizi kwenda Mzenga** magari yatasafiri muda wa mchana **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akitoa zawadi kwa Mwalimu Sophia Kawegere (kulia), baada ya kuibuka mshindi wa kwanza kwenye shindano la stadi za ufundishaji. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu TET, Dk. Aneth Komba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hoja 10 kutikisa mjadala bajeti ya serikali 2023/24

**Na Mwandishi Wetu**

WABUNGE leo wanaanza kuchambua na kujadili mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24, huku mambo 10 yakitarajiwa kutikisa mjadala huo.

Mjadala huo unafanyika baada ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2023/24, Alhamisi iliyopita, akiomba kuidhinishwa Sh. trilioni 44.39.

Hoja ya kwanza inayotarajiwa kutikisa mjadala huo, ni pendekezo la serikali kuongeza tozo katika ushuru wa saruji Sh. 20 kwa kilo. Pia kuongeza tozo ya Sh. 100 katika kilo lita ya mafuta ya petroli na dizeli. Tayari pendekezo hilo limenyooshewa kidole na wadau litaathiri wananchi wengi.

Eneo lingine ni ushuru katika nondo ambao ni Dola za Marekani 250 kwa ujazo wa tani moja. Nalo linatajwa litapaisha bei ya bidhaa hiyo.

Mapendekezo mengine ni yanayotarajiwa kuwa gumzo katika mjadala huo ni kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 kwa kila mita moja ya mraba ya marumaru, vyote vikiwa ni vifaa vya ujenzi ambavyo vinategemewa na Watanzania wengi.

Mjadala huo pia unatarajiwa kuelekezwa katika hoja ya ongezeko la ushuru wa asilimia 30 kwa tumbaku inayovutwa kwa kutumia bomba la maji na sigara za kielektroniki, shisha na bidhaa za aina hiyo.

Vilevile, pendekezo la serikali kuongeza kiwango cha asilimia 20 katika mashine za kamari zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na zinazozalishwa nchini.

Eneo lingine linalotarajiwa kuwa sehemu ya michango ya wabunge ni pendekezo la serikali kutoza kodi matangazo ya biashara mtandaoni hasa Instagram, Facebook, Twiter na Blogu mbalimbali yanayowekwa na watu maarufu.

Pendekezo lingine linalotarajiwa kuwa sehemu ya mjadala huo, ni la kufuta tozo kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Linatarajiwa kuungwa mkono na wabunge.

Wabunge pia wanatarajiwa kuunga mkono mapendekezo ya kuondoa, kupunguza kodi na tozo mbalimbali za ardhi ambazo zitawezesha Mtanzania wa kawaida kumiliki ardhi kisheria.

Pendekezo lingine linalotarajiwa kuungwa mkono na wabunge ni la kuondoa ada kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kupangiwa na serikali kujiunga na vyuo vya ufundi vya Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) ili kuongeza idadi ya wataalamu wenye ujuzi na elimu inayohitajika katika zama hizo za mapinduzi ya nne ya viwanda.

Hali kama hiyo inatarajiwa katika kuchangia pendekezo la serikali la kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya kati wanaochukua kozi za sayansi, afya na ualimu pamoja na kuongeza posho ya kujikimu 'boom' kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaopata mkopo wa elimu ya juu.

**HABARI KITAIFA**

# Mbowe aenda Uingereza na hoja nyeti ya kidemokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, anatarajiwa kushiriki kama mgeni maalum katika mjadala wa mwenendo wa kisiasa na mahitaji ya mabadiliko muhimu yatakayoimarisha amani na umoja Tanzania ulioandaliwa na Chatham House.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, kiongozi huyo ataondoka nchini leo kwenda Uingereza kwa ziara ya siku saba. Alisema kuwa akiwa Uingereza, Mbowe atahudhuria maadhimisho ya miaka 40 tangu kuasisiwa kwa Umoja wa Vyama vya Kidemokrasia Duniani (IDU) yanayofanyika leo jijini London. "Chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu mstaafu wa 22 wa Canada, Stephen Harper, ufunguzi wa maadhimisho haya unahudhuriwa na viongozi wanachama wa IDU vikiwamo vyama tawala na vya upinzani kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni vikiongozwa na viongozi wakuu wa vyama hivyo, miongoni mwao wakiwamo marais, mawaziri wakuu, wabunge, mawaziri walioko sasa madarakani na wastaafu," alisema.

Mrema alisema maadhimisho hayo yatafunguliwa na Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Boris Johnson.

Alisema kuwa akiwa Uingereza, Mbowe atashiriki kikao cha uongozi wa IDU Juni 21, mwaka huu, ambako yeye na Mwenyekiti Mwenza wa Umoja wa Vyama vya Kidemokrasia barani Afrika (DUA).

Katika mkutano huo, DUA watawasilisha taarifa juu ya hali ya demokrasia barani Afrika na uimarishwaji wa umoja huo.

"Ratiba ya Mheshimiwa Mbowe inahusisha pia vikao, mazungumzo na viongozi na mashirika mbalimbali ya maendeleo na demokrasia. "Atahitimisha ziara yake kwa kuzungumza na Watanzania wanaoishi Uingereza katika mkutano utakaofanyika Juni 24, mwaka huu na kurejea nchini Juni 25," Mrema alifafanua.

# Askofu Pengo atoa angalizo uendeshaji mpya wa Bandari

**Na Enock Charles**

ASKOFU Mkuu mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, ameishauri serikali kuwajengea uwezo wananchi, ili waendeleze miradi iliyopo nchini ukiwamo uendelezaji wa bandari kuliko kutegemea wawekezaji wa kigeni katika uwekezaji huo.

Akizungumza hivi karibuni na televisheni ya mtandao ya TEC kuhusu uwekezaji wa uendelezaji wa bandari ambao tayari umesharidhiwa na Bunge, Askofu Pengo alisema jambo jema kwa serikali yoyote duniani ni kuendeleza watu wake, ili baadaye wawe tegemeo katika masuala ya uwekezaji kuliko kuendelea kutegemea wawekezaji wa kigeni.

"Katika suala la bandari, bila shaka serikali inaona kuna kitu fulani cha kufaidi kutokana na kuleta mwekezaji kutoka nje, lakini mimi ninajiuliza hiyo itakuwa ni kusudi tupate fedha zaidi kuliko tunavyopata au ni kusudi kumfanya Mtanzania aendelee na awe na uwezo zaidi katika mazingira ya nchi yetu?" Askofu Pengo alihoji.

"Ningependa viongozi wetu wa serikali watambue kwamba jukumu walilonalo ni kumwendeleza Mtanzania. Mtanzania akishindwa, huwezi ukamtupa ukasema 'ninaweza kupata fedha nyingi zaidi kwa kumwacha huyu katika ujinga wake au katika uvivu wake akae huko. Mimi nitapata fedha zaidi kwa njia ya watu kutoka nje'. Kwanini umwache huyu Mtanzania abaki katika hali hiyo?" kiongozi huyo wa kiroho alihoji zaidi.

Jumamosi ya wiki juzi, Bunge lilipitisha azimio la mkataba wa uendelezaji bandari kati ya serikali na kampuni DP World ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano katika uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini baada ya wabunge kuchangia na kuishauri serikali kuhusu mkataba huo.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliuelezea mkataba huo kabla ya wabunge kuchangia na hatimaye kupitisha azimio hilo, akibainisha manufaa yake kwa taifa na kufafanua hoja zilizoibuliwa na wadau ikiwamo kuhusu muda wa utekelezaji na utatuzi wa migogoro na kampuni hiyo endapo ikitokea.

Kamati ya Bunge ya Miundombinu pia ilitoa ushauri katika maeneo mbalimbali kwa serikali, ikiwamo kuzingatia suala la ukomo wa muda katika mikataba itakayoingiwa, jambo ambalo linalalamikiwa na wadau kwamba makubaliano hayo hayajaonyesha ukomo wa muda.

## KUPOTEA KWA CHETI



**AWAMI HAMIS MOHAMED** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5029/0067** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PEHISCO SEKONDARI** mwaka **2019.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **NJO/MAK/RB/174257/2023.**


Compassion in Jesus' name

## Procurement Opportunities

### Advertisement for Pre-Qualification of Suppliers and Service Providers

Compassion International Tanzania (CIT) is part of Compassion International, Inc.-the worldwide Christian nongovernmental organization dedicated to child development and advocacy. CIT begun its operation in 1999. Twenty (20) years after the start, we have grown into one of the largest Christian child-focused, advocacy and development organizations in Tanzania. We are a child ministry pairing compassionate people with children living in extreme poverty to release the children from spiritual, economic, social, and physical poverty. In Tanzania Compassion International operates in 21 regions with its Head office in Arusha. CIT is inviting all interested suppliers across Tanzania to express their interest to supply and provide services to CIT as per description below: -

| | |
|---|---|
| Tender No: | PQ/CIT/001-2023 |
| Tender Name | Invitation for Pre-Qualification |
| Reference Number | CATEGORY A: SUPPLY OF GOODS |
| PQ/Goods/ CIT-001 | Supply of Office stationery. |
| PQ/Goods/ CIT-002 | Supply, repair and Maintenance of Electronics and Home Appliances |
| PQ/Goods/ CIT-003 | Supply and maintenance of ICT equipment ie. Photocopier, printer, UPS, etc. |
| PQ/Goods/ CIT-004 | Supply of branded items and promotional materials. |
| PQ/Goods/ CIT-005 | Supply, installation and maintenance of fire and security equipment and systems. |
| PQ/Goods/ CIT-006 | Supply of medicines for First Aids |
| PQ/Goods/ CIT-007 | Supply of office furniture and fixtures. |
| PQ/Goods/ CIT-008 | Supply of office upkeep i.e., tea bags, sugar, etc. |
| PQ/Goods/ CIT-009 | Supply of vehicles |
| PQ/Goods/ CIT-010 | Supply of News papers |
| PQ/Goods/CIT-011 | Supply and Servicing of Music Instrument |
| Reference Number | CATEGORY B: PROVISION OF SERVICES |
| PQ/Service/ CIT-001 | Provision of catering services (Arusha, Mwanza, Dodoma and Dar es Salaam offices) |
| PQ/Service/ CIT-002 | Provision of airtime (Mobile Voice & Data services) |
| PQ/Service/ CIT-003 | Provision of Air travel, reservations, and ticketing services. |
| PQ/Service/ CIT-004 | Provision of fumigation and pest control services. |
| PQ/Service/ CIT-005 | Provision of internet services. |
| PQ/Service/ CIT-006 | Provision of hotel accommodation and conference facilities. |
| PQ/Service/ CIT-007 | Provision of security services (guards) |
| PQ/Service/ CIT-008 | Provision of repair and maintenance of vehicles, motorcycles, and generators |
| PQ/Service/ CIT-009 | Provision of Building Repair & Maintenance Service (painting, plumbing, electrical etc.) |
| PQ/Service/ CIT-010 | Provision of Courier service |
| PQ/Service/ CIT-011 | Provision of Chartered plane service |
| PQ/Service/ CIT-012 | Provision of Translation Services |
| PQ/Service/ CIT-013 | Provision of Cleaning & Gardening services |
| PQ/Service/ CIT-014 | Provision of vehicle Tracking Services |
| PQ/Service/ CIT-015 | Provision of Vehicle Hire service |
| PQ/Service/ CIT-016 | Provision of printing services |
| PQ/Service/CIT-017 | Provision of Vehicle Insurance Service |
| PQ/Service/CIT-018 | Provision of part time staff for Data collection, Data Entry, drivers, receptionist etc. |
| PQ/Service/CIT-019 | Provision of video and photography services |
| PQ/Service/CIT-020 | Provision of TV and radio program airing services |
| Eligible Firms | National (Registered in Tanzania) |
| Method of Procurement | National Competitive Bidding |
| Mandatory Documents for submission | - Business License<br>- TRA documents (TIN/VRN certificate and Tax Clearance, proof of EFD)<br>- Regulatory body documents if applicable (TBS, TFDA, TMDA, TIRA, etc.)<br>- Registration/incorporation Certificate if applicable (BLERA)<br>- Company Profile (Among other things, state your coverage in Tanzania)<br>- Price list, delivery terms and payment terms.<br>- Evidence of similar work experience (Contract/Purchase orders)<br>- Business bank details (Acc name, number, bank name, providing bank statement is an added advantage)<br>- Official business address (Physical, post, email and phone number) |
| Mode of Application (Soft Copy) | Via Email, tzprocurement@tz.ci.tz<br>Please send all your documents in a single PDF file, indicate in your document and on the subject of your email, the category you are applying for; Your documents must be signed & stamped |
| Mode of Application (Hardcopy) | Olorien, Mtoto House, Plot No.18, P.O. Box 3064, Arusha Tanzania.<br>Pack your documents into a sealed envelope; your documents must be signed & stamped |
| Bids Submission | Effective 19th June 2023 to 06th July 2023 |



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

eGA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

# Majaliwa: Serikali imesikia kilio kodi kubwa taulo za kike

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imesikia kilio cha wadau kuhusu kuwapo kodi kubwa katika taulo za kike, akiahidi kufanyia kazi ili kuwainua wasichana na wanawake.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Shirika la WaterAid kwa Mwaka 2023-2028.

Majaliwa alisema serikali inatambua umuhimu wa kumwezesha mtoto wa kike hususani aliyeko shuleni kutimiza malengo yake ikiwamo kuwawekea mazingira rafiki ya upatikanaji wa taulo za kike.

"Nitamwagiza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuangalia namna ya kuondoa kodi katika taulo za kike. Yote yaliyozungumzwa na watoa mada, yote ilikuwa ni kodi kadhaa ambazo zinagusa maeneo ya vifaa vya usafi, kwamba viangaliwe tena," alisema.

Majaliwa alisema kwa kuwa vikao vya Bunge vinaendelea jijini Dodoma, atalifikisha kwa waziri mwenye dhamana ili katika bajeti yake alifanyie kazi.

"Wakati mjadala unaendelea wa kuikumbusha serikali kuzingatia ongezeko la bajeti katika Wizara ya Kilimo, Afya, Maji, kupitia wizara hizi zimepata ongezeko kubwa la bajeti. Hii ni mikakati ya serikali kila mwaka wa kuhakikisha utoaji huduma bora katika wizara hizi muhimu na nyeti," alisema.

Majaliwa alisema suala la usimamizi wa upatikanaji wa huduma za maji safi vijijini lipo katika mipango ya serikali.

"Hoja kwamba kwanini taulo za kike zisitolewe bure kama ilivyo kwa mipira ya kiume, ni kweli serikali inafanya kazi na sekta binafsi na mipira ya kiume inatolewa bure. Niwahakikishie serikali tumelichukua na tutalifanyia kazi ikiwamo kuondoa kodi japokuwa awali suala hili lilifanyiwa kazi," alisema Majaliwa.

Kwa kurejea, serikali iliamua kuondoa kodi katika taulo za kike miaka miwili iliyopita, lakini baadaye ilibaini kuwa uamuzi wake uliwanufaisha zaidi wafanyabiashara badala ya walengwa kutokana na kutoshushwa kwa bei ya bidhaa hizo. Katibu wa Jukwaa la Hedhi Salama (MHC), Severine Allute, alisema wamekuwa wakipigania kwa miaka mingi kuhusu upatikanaji, bei na uwezo wa watu kumudu kununua taulo za kike.

Alisema familia zinazoishi maisha duni hususani zinazopewa huduma na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) zinapaswa kupewa bure taulo za kike.

Allute alisema: "Hii ni bidhaa muhimu kwa mtoto wa kike, ni lazima ataihitaji katika maisha yake. Sasa kwanini itozwe kodi? Kwanini ipatikane kwa bei kubwa? Wafanyabiashara wanaifanya biashara bidhaa hii ilhali ni huduma muhimu."

Hivyo, aliiomba serikali kuliangalia upya kwa kuondoa kodi katika bidhaa hiyo sambamba na kuhakikisha inapatikana kwa bei rafiki na kwa familia zisizoweza kujimudu zipatiwe bure.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akikabidhi mkataba wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Bunge kwa Katibu wa Bunge ambaye ni Mwenyekiti wa baraza hilo, Nenelwa Mwihambi, baada ya kulizindua jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Mwanafunzi UDOM alituma ujumbe kwa mama yake kabla ya kunyongwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imeelezwa kuwa Happiness Fredrick, aliyekuwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), kabla ya kunyongwa na anayedaiwa mpenzi wake, alimtumia mama yake ujumbe mfupi kwa simu kuwa alikuwa na wakati mgumu, hivyo wamwombee.

Inadaiwa kuwa Machi 18, 2019 Happiness alinyongwa na Idrisa Mwakabola baada ya kijana huyo kuhisi anasalitiwa kimapenzi na binti huyo. Inadaiwa alimwekea kidonge cha usingizi katika juisi kisha kumnyonga.

Baba wa marehemu, Fredrick Francis (51), mbele ya Jaji Ephery Kisanya, akitoa ushahidi wake mwishoni mwa wiki, alieleza namna siku ya tukio mtoto wake alivyotoka nyumbani na kumpata akiwa maiti huku akiwa ameacha ujumbe kwa wadogo zake.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Upendo Mono, Francis alidai kuwa siku hiyo ya tukio, binti yake alitoka nyumbani akielekea Stendi ya Ubungo kwa ajili ya kukata tiketi ili kurudi chuoni mkoani Dodoma.

"Saa 10 jioni mimi nikiwa katika shughuli zangu, alinipigia simu na kunieleza kuwa basi alilotaka kusafiri nalo la Abood limejaa, basi alilopata ni Kimbinyiko. Basi nikamwambia akate hilohilo ili awahi chuoni.

"Kama dakika 15 zikapita nikasikia simu imeita kidogo ikakata, alikuwa Happiness, lakini nilipompigia haikupatikana. Baada ya saa mbili kupita nilimpigia mke wangu simu na kumweleza kuwa simpati mtoto kwenye simu, alinijibu kwamba bado hajarudi nyumbani," alidai Francis.

Aliendelea kudai kuwa aliporudi nyumbani saa moja usiku, mke wake alimweleza kuwa Happiness alikuwa hajarejea nyumbani, lakini wakajipa matumaini kwamba huenda alikuwa amekwenda kwa marafiki zake. Wakala na kapumzika.

"Ilipofika saa sita usiku, mke wangu akaniamsha kuwa mtoto hajarudi, nilishtuka sana! Nikamwambia nenda tena kaangalie chumbani kwake, lakini binti yangu hakuwapo. Tukaanza kumpigia simu, ikaita tu pasipo kupokewa.

"Wakati tunaendelea kutafuta jinsi ya kufanya, ujumbe mfupi uliingia katika simu ya mke wangu kutoka kwa Happiness kuwa yupo kwenye wakati mgumu sana, alisisitiza 'niombeeni na niagieni kwa wadogo zangu', lakini hatukujua kama ujumbe huo ulitumwa na mtoto wetu au mtu mwingine," aldai.

Alidai kuwa ujumbe huo, ulimshtua ndipo alipowapigia simu ndugu wa karibu wakafika nyumbani kwake kisha wakaenda Kituo cha Polisi Tandika, wakaturudishwa tena kituo kidogo cha Sigara ambako walielezwa kuwa kuna mwili wa binti uliokotwa.

"Tulikwenda Kituo cha Polisi Chang'ombe tukaambiwa twende Hospitali ya (Rufani) Temeke kuhakiki mwili uliookotwa saa 12 alfajiri. Kwa kuwa muda wa mochwari ulikuwa umeshapita, wakatuambia twende siku iliyokuwa inafuata kwa ajili ya utambuzi. Siku hiyo niliweza kumtambua mwanangu.

"Tulirudi tena kituoni hapo kwa ajili ya kupata kibali cha kuchukua mwili, tukaambiwa mwili unatakiwa kupelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya uchunguzi. Tulipofika, tulielezwa kuwa mtoto aliuawa kwa kunyongwa shingoni. Basi tukachukua mwili, tukazika," alidai.

# Sekretarieti ya Maadili yawaita wananchi kufichua viongozi waovu

**Na Joseph Mwendapole**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imewataka Watanzania kuisaidia kuwapata viongozi wa umma wanaokiuka maadili ya utumishi, ikiwahakikishia watakaotaja majina watalindwa kutokana na utendaji wake kuzingatia usiri.

Mwishoni mwa wiki, Katibu wa Sekretarieti Idara ya Ukuzaji Maadili, Yahaya Kipata, alitoa rai hiyo wakati wa mkutano baina ya sekretarieti hiyo na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam.

Alisema wananchi wanaweza kupeleka malalamiko ya viongozi hao kwa njia mbalimbali ikiwamo barua pepe, kwenda ofisi za sekretarieti au kwa njia ya simu.

Alisema taarifa watakazotoa kuhusu viongozi hao zitafanyiwa kazi na ikithibitika mhusika amekiuka maadili, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

"Msiogope kuleta malalamiko ya viongozi wala taarifa, tuleteeni taarifa. Jina lako litakuwa siri hautotajwa popote pale kwa sababu tunalinda watoa taarifa kwa mujibu wa taratibu zetu," alisema.

Alitaja baadhi ya hatua wanazochukuliwa viongozi wanaothibitika kukiuka maadili ya umma kuwa ni pamoja na kushushwa cheo, kulazimishwa kujiuzulu nafasi yake kazini na wakati mwingine kufukuzwa kazi.

Kiongozi huyo alisema kiongozi wa umma anaweza kukiuka maadili ya kazi yake kwa kujilimbikizia mali kinyume cha taratibu au kutumia ofisi yake vibaya kwa maslahi yake binafsi.

Kamishna wa Sekretarieti hiyo, Jaji mstaafu Sivangilwa Mwangesi, alisema hakuna ubishi kuwa suala la maadili limekuwa kilio cha kila kona nchini huku akiwaomba wadau mbalimbali kushirikiana katika kusimamia maadili hayo katika jamii.

"Maadili yamekuwa bidhaa adimu sana. Sasa ni namna gani tutalitatua tatizo hilo? Siyo suala la sekretarieti ya maadili peke yake, ni wajibu wa sisi sote wahariri na wananchi wote kwa ujumla tushirikiane tushauriane namna ya kukabiliana nalo," alisema.

Alibainisha kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kwa watu wa rika zote kuanzia vijana, wazee na viongozi wa umma kukiuka maadili na uadilifu, hivyo jamii inapaswa kushirikiana katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

"Tumeamua kuwaita ninyi ambao ndiyo mdomo wa jamii kwani mkijua sheria ya maadili ya viongozi wa umma mtatusaidia kutoa elimu kwa jamii yetu na hatimaye kurejesha uadilifu na maadili ambayo kwa kiasi kikubwa yameanza kuwa bidhaa adimu," alisema.

Alitaja baadhi ya misingi ya maadili ya utumishi wa umma kuwa ni kwa kiongozi kutotumia mali za umma kwa manufaa binafsi na kutoajiriwa sekta binafsi ambayo alikuwa na uhusiano nayo miezi sita baada ya kuacha utumishi wa umma.

Alifafanua kuwa baada ya kuacha utumishi, kiongozi wa Umma hatakiwi kuaibisha utumishi wa umma au kujinufaisha kwa kutumia utumishi wake uliopita na haruhusiwi kujipatia kwa makusudi manufaa ya kifedha au kumsaidia mtu mwingine kujipatia manufaa ya kifedha.

HABARI KITAIFA

# Chongolo alia na mila kandamizi kwa jamii

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka wazazi kuacha ukatili kwa kuendeleza mila za unyanyasaji, ukiwamo ukeketaji watoto wa kike.

Amesema jamii inapaswa kuachana na mila hizo na kuwapa fursa ya elimu watoto wa kike ili kuwasaidia katika maisha yao.

Chongolo alitoa rai hiyo jana alipotembelea na kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Chilonwa wilayani Chamwino katika mwendelezo wa ziara yake mkoani Dodoma.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka watoto wao shuleni na kuacha ukatili wa kuendeleza mila potovu za unyanyasaji wa wasichana kupitia vitendo vya ukeketaji.

"Bado kuna baadhi ya wazazi wanaendeleza ukatili wa kuendeleza mila potovu za ukeketa wasichana na wengine hawapeleki watoto wao shuleni. Hii ni hatari kwa maisha yao na kizazi kijacho," alisema.

Katibu Mkuu alisema kuendeleza mila hizo ni ukatili kwa wasichana kwa kuwa waliumbwa hivyo, wasitolewe viungo katika miili yao, wana haki ya kulindwa ili wasinyanyasike kwa vitendo hivyo.

Alisema watoto wanayo haki ya kupata elimu, hivyo kila mzazi ahakikishe anawapa nafasi kupata haki hiyo ya elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao ya baadaye. "Na kuna baadhi ya wazazi wamekuwa wanawazuia watoto kupata elimu na kuwapeleka kufanya kazi za ndani huko na wamekuwa wakinyanyasika kwa sababu hawana elimu," alisema.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa majengo ya shule hiyo, Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Chamwino, Tlinagwe Ngonile, alisema mradi huo wa ujenzi wa madarasa ya shule ya sekondari ni unahusisha majengo manane na unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 581.

Alisema fedha hizo zimetolewa na serikali na zitasaidia pia ujenzi wa matundu manane ya vyoo. Ujenzi wa ulianza Juni 5, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Agosti 5 mwaka huu.

Chamwino ni miongoni mwa wilaya zinazokabiliwa na uhaba wa shule za kidato cha tano nchini. Ofisa Elimu huyo alisema shule hiyo ina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne, hivyo kukamilika kwa majengo hayo kutasaidia wanafunzi wa Tarafa ya Chilonwa kupata elimu ya kidato cha tano na sita shuleni hapo. Mbunge wa Chilonwa, Deogratius Ndejembi, aliishukuru serikali kwa kuwapatia vifaa tiba ambavyo vimesaidia kuondoa kero ya huduma ya upasuaji iliyokuwa inaikabili Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Ndejembi alisema kuna tatizo la uhaba wa mabweni kwa wanafunzi wasichana ili kuwakinga dhidi ya mimba za utotoni.

# UDBS yawajengea uwezo vijana kujiajiri

**Na Mary Geofrey**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kupitia Shule Kuu ya Biashara (UDBS), Idara ya Fedha, kimeendelea kuwajengea uwezo wanafunzi kupitia majukwaa ya kibenki, fedha na uwekezaji ili wanapohitimu masomo yao, wajiajiri na kushindana katika soko la ajira duniani.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni wa wiki katika Jukwaa la Tano la Kibenki, Fedha na Uwekezaji, Mkuu wa Idara ya Fedha, Dk. Tobias Swai, alisema kupitia majukwaa hayo, wanawawezesha wanafunzi kupata taarifa sahihi kuhusu masuala ya kibenki, fedha na uwekezaji.

"Majukwaa kama haya yamekuwa yanaleta chachu kwa wanafunzi kwani yamewakutanisha na wataalamu wabobezi na wadau mbalimbali kujadili mada, changamoto na kuainisha fursa zilizopo katika sekta ya fedha," alisema Dk. Swai.

Dk. Swai alibainisha kuwa dhima nzima iliyobeba jukwaa hilo ni kutambua changamoto na fursa katika uendeshaji wa taasisi ndogo za kifedha nchini.

Alitoa rai kwa wadau katika sekta hiyo kuendelea kujitoa kwa hali na mali katika kukuza na kueneza elimu ya fedha na uwekezaji hususani kwa vijana kwa manufaa ya sasa na kizazi kijacho.

Mkuu wa Biashara kutoka TIB Rasilimali Limited, George Sawe, alisema elimu ya mambo ya fedha na uwekezaji inapaswa kutolewa kwa wanafunzi ili kuwajengea utaratibu wa kuwekeza katika masoko ya kifedha na hivyo kukuza kipato chao. "Tutaendelea kushirikiana kwa karibu na UDSM ili kuendelea kutoa elimu kwa wanafunzi juu usimamizi wa fedha na uwekezaji ili sekta hii ya fedha ikatoe mchango stahiki katika kukuza Pato la Taifa," alisema Sawe.

# RC aagiza wakaguzi wapewe ulinzi baada kuibuka vitisho

**Na Moses Ng'wat,** TUNDUMA

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, ameliagiza Jeshi la Polisi wilayani Momba kuwapa ulinzi Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Mji Tunduma na msaidizi wake kutokana na vitisho walivyoanza kuvipata baada ya kutoa ripoti ya ukaguzi iliyosababisha watumishi sita wa halmashauri hiyo kuchukuliwa hatua, ikiwamo kufukuzwa kazi.

Alitoa agizo hilo Juni juzi wakati wa kikao cha Baraza Maalum la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma kilichoitishwa kwa lengo la kujibu hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22.

Aliagiza Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri hiyo, Engelbert Maro na msaidizi wake, Thomas Mzee, wapewe ulinzi kwa kuwa ana taarifa watendaji hao wameanza kupewa vitisho na kumtaka Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD), John Lwamlema, kutekeleza agizo hilo mara moja.

"Kamanda wa Polisi Mkoa leo (juzi) hatuko naye hapa, lakini wewe OCD uko hapa. Ninataka huyu Mkaguzi wa Ndani na msaidizi wake uhakikishe wanalindwa... maana nina taarifa wanatishwatishwa.

"Nichukue nafasi hii kuwapongeza wewe Mkuu wa Idara ya Ukaguzi na mwenzako... yule rafiki yangu (Thomas Mzee) mmefanya kazi nzuri sana katika ripoti yenu ya ukaguzi kwa sababu kuna watumishi wanafikiri fedha zinazoletwa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni za kugawana," alielekeza.

Wiki iliyopita, Baraza hilo la Madiwani liliwafukuza kazi watumishi sita, huku wengine wawili wakikumbwa na adhabu ya kukatwa asilimia 15 ya mishahara yao kwa kipindi cha miaka mitatu baada ya kupatikana na makosa mbalimbali yakiwamo ya ubadhirifu.

Baraza hilo pia lilimshusha wadhifa Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Halmashauri hiyo, Ronald Msangi, huku watumishi wengine wanne wakinusurika baada ya baraza kujiridhisha hawakuwa na hatia katika makosa yaliyokuwa yanawakabili.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ayoub Mlimba, aliwaambia wandishi wa habari kuwa walifikia uamuzi huo kufuatia hoja zilizoibuliwa na madiwani katika kikao cha baraza cha mwezi Desemba mwaka jana.


**TANZANIA CONCRETE POLE MANUFACTURING COMPANY LIMITED**

TCPM

**EMPLOYEMENT ADVERTISEMENT – PROJECT MANAGER**

Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited (TCPM) is a Public Company which was incorporated in 16th December 2014 as a subsidiary Company of Tanzania Electricity Supply Company Limited (TANESCO) and became operational in September 2017.

The Company's primary objective is to carry out the business as promoter, developer, consultant, advisor and investor in the concrete poles manufacturing by providing commercial, engineering, financial, environmental, asset management, technical due diligence, technological assessment, supervision, specifications, construction supervision and testing and quality control, training and capacity building in concrete poles manufacturing technologies. TCPM is looking for a suitable qualified person to fill the post of Project Manager on Contract for 2 years (renewable on performance).

**Job Purposes**

Developing detailed project plans, ensuring resource availability and allocation and delivering every project on time within budget and scope.

**Key Responsibilities**

- Advise General Manager on all matters pertaining to projects management and Public Private Partnership for effective performance of the Company
- Coordinate with major related investors to ensure the Company entered into Public Private Partnership agreement.
- Coordinate internal resources and third parties' resources for the sound execution of projects.
- Conduct comprehensive research and feasibility studies for various projects proposals to ensure all project undertaken are viable.
- Identify project risks and implement mitigation strategies to ensure successful project completion.
- Define project scope, goals and deliverables that support business goals in collaboration with management, other stakeholders and ensuring technical feasibility.
- Effectively communicate project expectations to team members and stakeholders in a timely and clear fashion.
- Plan and schedule project timelines and milestones using appropriate tools.
- Track project milestones and deliverables.
- Define project success criteria and disseminate them to involved parties throughout the projects life cycle.
- Conduct project postmortems and create a recommendations report identifying successful and unsuccessful project elements.
- Estimate the resources and participants needed to achieve project goals.
- Draft and submit budget proposals, meet budgetary objectives and recommend subsequent budget changes where necessary based on financial analysis.
- Ensure that at all times the company is getting best value for money for all projects spend by strong commercial management and rigorous cost control.

**Qualifications**

Holder of Bachelor Degree in Business Administration, Finance, or Economics. Must have a Master Degree in Business Administration, Finance, or Economics and Project Management Professional (PMP) Certification with a minimum of five (5) years of relevant project management working experience and proven good performer.

**Personal Attributes**

- Visionary
- Integrity
- Analytical thinking
- Leadership skills
- Innovative and creative
- Excellent Communication skills
- Capable of strategic engagement with key local and international stakeholders.
- Problem Solving
- Formulating strategies and concepts
- Deciding and initiating action
- Strong influencing and negotiating skills
- Relationship management at executive level
- Commercial awareness
- Planning and organizing
- Extensive Project Management skills-PMBOOK

**General Information.**

The contract for the position is for two-years renewable subject to performance and availability of funds.

**Applications.**

Application letter including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address and address and telephone number of two referees should be sent to the General Manager, TCPM, P.o. Box 31438, Dar es salaam. Please note that only shortlisted candidates will be contacted. **Closing date 3rd July 2023.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuiunge mkono Taifa Stars kufuzu AFCON

**TIMU** yetu ya soka ya Taifa 'Taifs Stars' jana ilicheza mchezo wake muhimu wa kuwania kufuzu fainali za Afrika za mwakani zitakazofanyika Ivory Coast kuanzia Januari 13.

Taifa Stars ilifanikiwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Niger na kufufua matumaini ya kufuzu kushiriki fainali hizo kwa mara ya tatu.

Ushindi wa jana bila kuangalia matokeo ya Uganda waliocheza jioni dhidi ya Algeria, ulifufua matumaini ya Stars kufuzu kama itafanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo wa mwisho dhidi ya Algeria utakaochezwa baadaye mwaka huu.

Bado msisimko kwa timu yetu ya taifa upo chini ukilinganisha na klabu zetu zinapocheza mchezo wa kimataifa au mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Jana hakukuwa na idadi kubwa ya watu kama ilivyozoeleka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuishangilia timu yetu.

Taifa Stars ni timu yetu bila kujali ushabiki wowote, linapokuja suala la kitaifa ni lazima tuiunge mkono timu yetu ambayo inatuwakilisha kwenye mashindano mbalimbali inayoshiriki.

Ndani ya Taifa Stars hakuna Usimba wala Uyanga, wote tunapaswa kuwa kitu kimoja na kujitokeza kwa wingi kuisapoti pale inapocheza kwenye uwanja wa nyumbani.

Mpaka kufikia sasa imebakisha mchezo mmoja kwenye kundi lake dhidi ya Algeria, ni mchezo muhimu utakaotoa nafasi kwa Stars kuweza kufuzu kwenye fainaliza mwakani za AFCON.

Kama Watanzania na tukithamini cha kwetu, tuiunge mkono timu yetu ili imalize vizuri michezo yake na kufuzu kwa fainali za mwakani zitakazofanyika Ivory Coast.

Michezo ya mwisho kwenye kundi F, wakati Stars ikicheza na Algeria, wapinzani wetu wakubwa Uganda itacheza na Niger kusaka tiketi ya kucheza AFCON mwakani.

Hapa ndipo tunapotakiwa kuungana kama nchi na kusapoti timu yetu kuweza kufuzu kwa fainali za Afrika na kuwa mara ya tatu kushiriki fainali hizi.

Wachezaji wetu wanahitaji sana sapoti yetu kama mashabiki na kama wananchi wa taifa hili la Tanzania, kwa pamoja tukiungana kama nchi tukaiunga mkono timu yetu, inaweza ikafuzu kwa fainali hizi.

Tuiunge mkono timu yetu lakini pia tumuunge mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan ambaye ameonyesha kuwa na mapenzi makubwa na mpira wa miguu.


Rais Samia ameonyesha mapenzi yake kwenye soka hasa baada ya kuziunga mkono klabu zetu mbili za Simba na Yanga wakati wakishiriki mashindano ya kimataifa.

Kufanya vizuri kwa Taifa Stars ni wazi kutamfurahisha Rais wetu na haitashangaza kuiunga mkono pale itakapocheza michezo yake ya kimataifa.

Tuna uhakika Taifa Stars inauwezo wakufuzu kwenye fainali za AFCON, kama wananchi tunapaswa kuiunga mkono kuweza kufikia malengo yake ya kucheza kwa mara ya tatu fainali hizo.

Kwenye soka hakuna kinachoshindikana, tunaitakia kila la heri timu yetu kwenye mchezo wake wa mwisho dhidi ya Algeria ambao utatupa uhakika wa kufuzu kwenye fainali za mwakani za AFCON.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mashabiki wanavyolia na kanuni za Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**TANGU** Juni 7, Bodi ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara (TPLB) imekuwa ikikusanya maoni ya maboresho ya kanuni za Ligi Kuu, Championship na 'first league' kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa 2023/24.

Idara ya Habari na Mawasiliano ya bodi hiyo, ikasema lengo la kufungua dirisha hilo ni kukusanya maoni kwa ajili ya kutengeneza kanuni zitakazotumika kwa ajili ya msimu ujao.

Maoni hayo wanayahitaji kutoka kwa wadau wa mpira wa miguu hususan ligi hizo tatu ili kupata mawazo mapya ya namna ya kuendelea kuboresha uendeshaji na usimamizi wa ligi.

Taarifa hiyo ikawataka wadau mbalimbali zikiwamo klabu za mpira wa miguu, mashabiki, wanahabari, vyama vya mpira wa miguu, wadhamini, taasisi za kiserikali na binafsi kuwasilisha mapendekezo yao kabla ya usiku wa Juni 30, 2023. Leo ndiyo kwanza Juni 19, kwa hiyo muda bado upo.

Bodi ikawataka wadau watakaokuwa na maoni yao kuyawasilisha kwa mkono kwenye ofisi za Bodi ya Ligi Kuu Tanzania zilizopo ghorofa ya 14 ya jengo ya NSSF (Mafao House), Ilala Boma, Dar es Salaam, au kupitia anwani ya barua pepe Maoni@ligikuu.co.tz, kabla ya saa 5:59 usiku wa Juni 30, 2023.

Tayari wadau wengi wamekuwa wakitoa mawazo yao na kuyapeleka kwa njia mbalimbali ambazo wanaona zinafaa.

Hata hivyo kuna kundi kubwa la mashabiki wa soka wana mawazo mengi mazuri lakini hawajui kwa kuyawasilisha.

Wengine hawawezi kuwasilisha kwenye barua pepe, wala kupeleka kwa mkono kwenye ofisi za bodi, lakini wamekuwa wakiyatoa vijiweni, maofisini, kwenye majukwaa mbalimbali yanayozungumzia soka na mengine yanayofanana na hayo.

Nimekuwa nikipita sehemu mbalimbali na kukutana na mashabiki wengi ambao wana maoni na hawawezi kuyawasilisha kwa sababu mbalimbali, ikiwamo muda, nauli, uelewa na kadhalika.

Hata hivyo wana mawazo chanya ambayo kama nayo Bodi ya Ligi wakiyasoma hapa na kuyafanyia kazi kuyaingiza kwenye mchakato wanaweza kutoka na kitu ambacho kitawasaidia kutopata lawama msimu ujao.

Kila msimu limekuwa likitokea jambo ambalo linazua utata na mashabiki kuanza kulaumu, japo maoni haya hutolewa kila msimu baada ya kumalizika kwa msimu wa mashindano yanayosimamiwa na Bodi hiyo ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Kwa mfano kuna suala lililotokisa la ufungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara lililomalizwa kwa Kamati ya Tuzo kuwapa tuzo wachezaji wote wawili, Saido Ntibazonkiza wa Simba na Fiston Mayele wa Yanga kwa kupachika mabao 17 kila mmoja.

Wengi niliowasikiliza walikubaliana na mawazo ya Rais wa TFF, Wallace Karia kuwa tuzo iwe moja kwa mfungaji hata kama wamefunga mabao sawa kwa kuangalia vigezo vingine.

Lakini hawataki kiwe ni kufunga mabao ya penalti au 'assist' nyingi kwa sababu hiyo ni tuzo ya ufungaji bora, si vinginevyo.

Wakadai hata penalti ni mabao tu, na mchezaji asikose taji kwa sababu amefunga mabao mengi ya tuta kwani nao ni ufundi na mpira kwa sababu si kila mtu anaweza kupiga na kufunga.

Wengi wanataka kama ikitokea wakiwa sawa kwa mabao, basi mfungaji bora awe ana 'hat-trick' nyingi kuliko mwenzake. Na kama wakiwa wanazo sawa, basi iangaliwe yule aliyefunga mabao mengi kwenye mechi moja kwa sababu kuna wengine wanafunga hata mabao manne au matano kwenye mechi moja. Kigezo cha kwanza kiwe 'hat-trick' kama ana mbili na mwenzake moja, basi mwenye nyingi ndiye awe mfungaji bora.

Kingine wanataka klabu mwenyeji asichukue mapato yote ya mlangoni, badala yake mgeni apate japo asilimia 40 kwa sababu viongozi wanaingia gharama za kusafirisha timu kwenda ugenini, zingine zikitumia usafiri wa ndege, lakini haziambulii chochote, huko na kuzinyonya baadhi ya klabu.

# AICT yawakumbusha waumini kukeme ndoa jinsia moja

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAKAMU wa Askofu Mkuu wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT), Jimbo la Shinyanga, Zakayo Bugota, amewataka waumini pamoja na wachungaji wa kanisa hilo kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kukemea na vikali uwapo wa vitendo vya ndoa za jinsia moja katika jamii.

Askofu Bugota alitoa kauli hiyo jana wakati wa hafla fupi ya kuweka jiwe la msingi katika nyumba ya kiaskofu ya Dayosisi teule ya Kahama iliyojengwa kwa nguvu za waumini, iliyopo Mtaa wa Shunu, Kata Nyahanga Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na kusema kuwa ni wakati wa kanisa kusimama na kukemea vitendo hivyo viovu.

Alisema wachungaji wanatakiwa kutumia nafasi zao katika ibada na mahubiri yao kukemea ili kunusuru kizazi cha sasa kwa manufaa ya taifa la kesho

"Sisi maaskofu na waumini wa kanisa hili la AICT tusimamie maadili mema na kuyakemea yale yote ambayo yanamchukiza Mungu hasa hili la ndoa la njia moja, kwanza linafanywa na watu wasiokuwa na uadilifu hivyo ni wajibu wetu kuyakemea kila tunapofanya ibada zetu," alisisitiza Askofu Bugota.

Suzani Oke ni mmoja wa waumini wa kanisa hilo alisema kuwa suala la ndoa za jinsia moja limekuwa tatizo kubwa ndani ya jamii na ili kukabiliana nalo inatakiwa serikali kuweka maadhimio ya nini kifanyike hasa pale watu watakapobainika kujihusisha na masuala hayo na kuwabana wale wanazifungisha.

Naye Emmanuel Madeleke alisema, viongozi wa dini bila kujali itikadi za kidini wahakikishe suala la maadili linakuwa ajenda ya kudumu katika ibada zao, na kuwasisitiza wanafamilia hasa wazazi wa kiume kutenga muda wa kuzungumza na watoto ili kutatua changamoto zinazowakabili kwani wengi wanatendewa maovu mitaani, lakini hawasemi.

Awali akisoma risala ya ujenzi wa nyumba hiyo, John Mtumayi alisema, ujenzi wa nyumba ya Askofu wa Dayosisi teule ya Kahama, umefikia asilimia 80 kwa zaidi ya Sh. milioni 100 fedha kutokana na nguvu za waumini na kufika Agosti, mwaka huu itakuwa imekamilika na kuanza kutumika.

Alisema, mpaka sasa kanisa limejipanga kuanzisha ujenzi wa taasisi mbalimbali za elimu na afya kwa kujenga shule ya msingi, sekondari na zahanati kama sehemu ya vyanzo vya mapato ya dayosisi hiyo na kuwaomba waumini kushirikiana na kutimiza hayo kwa wakati ambao watakuwa wameupanga kupitia vikao.




Mkurugenzi wa Wakala wa Mkongo Zanzibar (ZICTIA), Shukuru Awadh Suleiman (katikati) pamoja na Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani wa Vodacom Tanzania PLC, Brigita Shirima (wa pili kulia), wakikata utepe wakati wa uzinduzi wa mnara wa mawasiliano wa Vodacom Tanzania katika mji wa Makunduchi, uliopo ndani ya Mkoa wa Kusini Unguja jana. Kutoka kushoto ni Meneja Mauzo Mwandamizi, Liston Chale, Katibu Tawala Wilaya ya Kusini - Unguja, Baraka Omary Kaengeo na Meneja Mauzo, Fadhili Linga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashirika 8 yafanya matembezi kulaani ucheleweshaji mabadiliko Sheria ya Ndoa

**Na Elizabeth Zaya**

MASHIRIKA manane yasiyo ya kiserikali likiwamo la Msichana Initiative, C-Sema, Flaviana Matata, Jamii Forum na Tai Tanzania, yamefanya matembezi ya kulaani mwendelezeo wa ucheleweshwaji wa mabadiliko ya vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 wakidai ni uvunjifu wa sheria na Katiba ya nchi.

Vifungu hivyo vinaruhusu mtoto wa kike kuolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa matembezi hayo yaliyofanyika Dar es Salaama ikiwa ni kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, walisema ni miaka minne sasa tangu Mahakama ya Rufani kutamka bayana kwamba vifungu hivyo vinavunja Katiba kwa kuvunja haki na usawa.

"Mahakama hii ilitoa maagizo kwa serikali kuvifuta vifungu hivi na kwamba kazi hiyo ilipaswa kukamilika ndani ya mwaka mmoja toka siku ya agizo lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika," alisema Alice Mtuga wa Jukwaa la Utu na Mtoto (CDF).

"Inasikitisha kuona serikali ambayo inapata mamlaka yake toka katika Katiba na sheria za nchi, inaweza kuzifiginya sheria hizo kwa kupuuza agizo la mahakama. Kama wananchi na wapenda haki tunalaani kitendo hiki cha uvunjifu wa sheria na katiba ya nchi."

Mwakilishi kutoka Shirika la C-Sema, Jane Haule C-Sema, alisema zaidi ya asilimia 30 ya wasichana nchini huolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18.

"Takwimu hizi ni kwa mujibu wa 'Demographic and Health Survey, Malaria Indicator Survey 2016'. Pia kwa Mujibu wa Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Tanzania inashika nafasi ya 11 duniani kwa kuwa na idadi kubwa watoto wanaoolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 18."

Mwanafunzi wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Kitunda, Tonny Yohana, alisema sheria hiyo inakatisha haki ya kielimu hasa kwa watoto wa kile ambao wao ndio huozeshwa katika umri mdogo na kukatisha ndoto zao.

"Kwa hiyo tunaiomba serikali iondoe hiyo sheria ili watoto wa kike nao wapate fursa ya kutimiza ndoto zao kielimu maana tumekuwa tukishuhudia hata ndugu zetu wa kike wakiathirika na suala hili," alisema Tonny.

Nisela Pastory, mwanafunzi wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Tandika, aliiomba serikali kuwalinda watoto wa kike kwa kudhibiti vitendo vya ukatili dhidi yao ikiwa ni pamoja na kufanyia marekebisho vifungu vinavyoruhusu mtoto kuozeshwa chini ya umri wa miaka 18.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# Mtaka akaribisha watalii Pori la Mpanga Kipengere

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, amesema upekee wa Pori la Akiba Mpanga Kipengere ni maporomoko makubwa ya maji Afrika ambayo yanatiririka mwaka mzima.

Pori hilo liko katika mikoa miwili, sehemu kubwa iko mkoani Njombe katika wilaya ya Makete na Wanging'ombe na sehemu iliyobaki ikiwa ndani ya Mkoa wa Mbeya.

Mtaka aliyasema hayo baada ya kufanya utalii katika pori hilo na maadhimisho ya Siku ya Maporokomo Duniani kitaifa mkoani humo.

"Kuna mambo matatu, moja ni kutangaza eneo la Mpanga Kipengere kama eneo la utalii ndani ya mkoa, Watanzania wajue kwamba Njombe tunalo pori la akiba, upekee wa pori hili tofauti na mapori mengi ya akiba kama Maswa, Kigereshi, ni kwamba pori hili lina maporomoko ya maji ambayo kwanza ni ya mwaka mzima, lakini pili ni maporomoko makubwa sana kwenye ukanda wa Afrika," alisema Mtaka. "Mtu kama anataka kuandika mambo yake ya maisha, anataka kuandika kitabu, anataka kuandika mirathi anataka kuandika mambo yanayohusu familia, Mpanga Kipengere kwenye eneo hili la maporomoko maji ni eneo lenye utulivu sana," alisisitiza Mtaka.

Alitoa rai kwa wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo ya utalii badala ya kukimbilia mijini.

"Tunatoa fursa kwa Watanzania tutoke kwenye kasumba ya kuona hoteli za kitalii zinajengwa na watu kutoka nje bado tunao Watanzania ambao wanaweza kufanya uwekezaji ule ule wa Njombe Mjini Makambako, Mbeya, Igawa akaja akafanya uwekezaji wa hoteli," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alisema sekta ya utalii inachangia asilimia 17 ya pato la taifa na asilimia 25 ya fedha ya kigeni ambayo inatumika kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mkuu wa Hifadhi ya Mpanga Kipengere, Donasiani Makoi, alisema maadhimisho hayo yameletwa Njombe kwa sababu hifadhi hiyo, Tanzania, Afrika Mashariki na AfriKa ndio yenye maporomoko mengi ya maji.

Makoi alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha utalii kwa Nyanda za Juu Kusini Kama Rais Samia Suluhu Hassan alivyofanya kwenye filamu ya Royal Tour.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omary, alisema Mkoa wa Njombe una maporomoko mengi na kwamba atawasimamia wakurugenzi wa halmashauri ili kuyasimamia na kuyaboresha ili yawe kivutio.

Balozi wa utalii Tanzania Bongo Zozo, akizungumza na Nipashe aliwapongeza pori la akiba Mpanga Kipengere kwa kutunza mazingira na kulinda usalama kwenye hifadhi hiyo.



Mmoja wa wazazi wa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Urafiki Dar es Salaam, akichangia mada katika kikao cha kujadili malezi bora na namna ya kupambana na rushwa ya ngono, ukatili wa kijinsia na ndoa za utotoni. Kikao hicho kiliandaliwa na Shirika la Usawa wa Kijinsia Tanzania (SUKITA) juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Malima azionya h'shauri ukataji miti ovyo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, amezionya halmashauri zote za mkoa huo kuacha kutegemea mapato yanayotokana na kuni na mkaa.

"Mimi nakuombeni wakurugenzi wangu kwa usalama wenu wenyewe, asitokee mtu kuniletea taarifa ya mapato yanayotokana na kuni na mkaa nyie mkifanya hivyo ndio mtakuwa maadui wangu wa kwanza," alisema.

Amewataka wakurugenzi hao kuhamasisha halmashauri zao kuchangamkia fursa ya kupata mapato yanayotokana na uvunaji wa hewa ukaa kwa kutumia misitu watakayohifadhi katika maeneo yao.

Alitoa onyo hilo, wakati akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Morogoro, katika uzinduzi wa kampeni ya utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi na salama, inayoendeshwa na kampuni ya Taifa Gas.

Alisema amebaini uharibifu mkubwa wa misitu hasa ukataji miti na uchomaji wa mkaa Mkoa wa Morogoro na kuwataka wanaohusika kuacha mara moja.

"Nimefanya ziara katika wilaya zote za Mkoa wa Morogoro, katika pitapita nimegundua misitu mingi imeharibiwa ndani kwa ndani, nje unaona misitu ipo na shughuli kubwa ni ukataji wa kuni na kuchoma mkaa sasa hii ni hatari kwa siku za usoni kwa tishio la uko miaka ya mbele ya kuhatarisha mkoa wetu na mimi sitokubali hilo litokee," alisema.

Kuhusu mapato yanayotokana na hewa ukaa hapa, alisema ipo halmashauri moja ya Tanganyika iliyopo mkoani Katavi imehifadhi misitu iliyofunga vizuri na inajipatia Shilingi bilioni tatu kwenye mauzo ya hewa ukaa na kutaka halmashauri za Mkoa wa Morogoro kuiga.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kutumia nishati ya gesi badala ya mkaa na kuni ambazo ndio chanzo kikubwa cha uharibifu huo wa misitu.

Alisema kwa Mkoa wa Morogoro gunia la mkaa ni 50,000 ambayo ni wastani wa matumizi ya gunia moja kwa mwezi inayolingana na ujazo wa gesi wa kilo sita ambayo huuzwa Sh. 23,000 na matumizi ni rahisi kuliko mkaa.

Alisema wakati wanapambana kuzuia matumizi hayo ni lazima wawe na kampuni ya nishati ya gesi ambayo itawahakikishia upatikanaji wa nishati hiyo kwa bei nafuu.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Taifa Gas, Angela Bokhe, alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali za kupunguza ukataji wa miti na uchomaji wa mkaa wameanzisha kampeni ya kupambana na hali hiyo ili kulinda misitu.

Alisema katika kampeni hiyo watatoa bure mitungi 5,000 kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro ili waache matumizi ya mkaa na kuni ili misitu ya Mkoa wa Morogoro ambayo ndio tegemeo kubwa matumizi ya maji kwa wakazi takribani milioni 10 wa mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro iweze kupona.

Angela alisema katika kutekeleza agizo la serikali la kuzitaka taasisi zote kutumia nishati ya gesi, wametengeneza matangi ya kupikia ya tani kuanzia moja hadi tano yenye thamani ya shilingi milioni saba ambayo yatatolewa bure kwa taasisi ili kuwarahisishia kuingia katika mfumo huo.

Akizungumzia manufaa ya nishati ya mpango wa kutumia nishati safi na salama, Mkuu wa Chuo cha Ualimu Morogoro, Augustine Sahili, alisema matumizi ya gesi ni nafuu na salama kuliko kuni na mkaa kwa kuwa unapika kwa muda mfupi.

# TBS yakabidhi zaidi ya vyeti 200 vya kuthibitisha ubora

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limekabidhi vyeti na leseni 264 vya kuthibitisha ubora wa bidhaa kwa wafanyabiashara mbalimbali na vyeti saba vya kuthibitisha ubora wa mifumo.

Vyeti na leseni hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki kwa wazalishaji ambao bidhaa zao zimethibitishwa kukidhi matakwa ya viwango kwa kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba, 2022 hadi Mei, 2023. Akizungumza kwenye hafla hiyo, ambayo ilifanyika Makao Makuu ya TBS jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema leseni na vyeti 107 ambayo ni sawa na asilimia 41.6 vilitolewa kwa wajasiriamali wadogo.

Alisema vyeti na leseni zilizotolewa ni za bidhaa za vyakula, vipodozi, vifaa vya ujenzi, vilainishi, vifaa vya umeme, trela, vibebeo, vifungashio pamoja na mifumo ya utoaji huduma.

Aidha, alisema kwa kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba 2022 mpaka Mei, 2023 wamesajili maeneo (maduka, maghala, magari) 1,394 ya kuuza, kuhifadhi na kusambaza bidhaa za vyakula na vipodozi.

Pia, alisema kwa kipindi hicho wamefanikiwa kusajili bidhaa 1,255 za vyakula na vipodozi kutoka nje ya nchi.

Dk. Ngenya aliwasisitizia wajasiriamali hao kuwa mabalozi wazuri katika matumizi ya viwango ili kufikia lengo la Tanzania ya viwanda hasa katika kipindi hiki Tanzania ikiwa uchumi wa kati.

Hafla hiyo ilibeba kaulimbiu ya ubora ya mwaka huu wa 2022/2023 inayosema "Dhamira bora fanya kwa usahihi" ambayo ni kwa wazalishaji kuwa ubora wa bidhaa unaanza na nia njema ya kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

Dk. Ngenya alisema wajasiriamali wanapaswa kuzingatia kanuni na miongozo iliyopo kwa hiari na kwa usahihi ili watumiaji wapate bidhaa bora muda wote.



# Kesi za ndoa, talaka zawa shubiri wilayani Moshi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KESI za ndoa na talaka zinazopelekwa katika mabaraza ya usuluhishi ngazi ya kata zimegeuka tishio Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, ikielezwa kundi lililoathirika zaidi na migogoro hiyo ni la miaka 35 hadi 50.

Aidha, inaelezwa wanandoa hao wanapokwenda katika mabaraza hayo, wengi wao huwa tayari walishachukua uamuzi mgumu wa kujiandika talaka na wanapofika barazani, huwa hawataki usuluhishi zaidi ya fomu namba tatu ya Mahakama inayohusu takala.

Wajumbe hao walifichua siri hiyo jana wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika la KWIECO, linaloendesha mradi wa majaribio wa utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya kifamilia, nje ya vyombo vya Mahakama na polisi, unaotumia njia mbadala za utatuzi na usuluhishi wa migogoro (ADR).

Mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Legal Service Facility Tanzania (LSF).

Mjumbe wa Baraza la Usuluhishi Kata ya Uru Kusini, Aurelia Njau, akizungumzia changamoto hiyo alisema: “Wanakuja kwetu wakiwa tayari kila mtu ameshaanda hatma yake kwamba hapa tumefika hitimisho, hatutaki tena ndoa. “Kwa hivyo, kila unapomsuluhisha unamwambia kubalianeni pale mlipotoka, mlipoanzia mapenzi yenu hebu jaribuni kujishusha. Ukimwambia kaka jishushe au dada jishushe, anakupa karatasi, anakwambia hapa ndoa ni mapenzi, hakuna tena mwanzo, wala mwisho, tumefikia mwisho.

Aidha, mjumbe mwingine wa baraza la usuluhishi, Flomena Kway, alisema hivi sasa wanapitia wakati mgumu, kwa kuwa wanandoa wanaokwenda kwenye mabaraza hayo hawataki kusuluhishwa na kuridhiana, wao lengo lao kuu ni talaka.

Akitoa maelezo kuhusu mafunzo hayo, Mratibu wa Mradi wa ADR, Lilian Mandari, alisema hadi kufikia sasa wameshawafikia wasaidizi wa kisheria 173, kwa sasa wanaendelea kutoa elimu hiyo kwa mabaraza ya kata.

Baada ya maelezo hayo, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Muhsin Kilua, aliwaeleza wajumbe hao kuwa, mfumo huo wa utatuzi wa migogoro una manufaa kadhaa ikiwa ni paamoja na uwepo wa taratibu rafiki na rahisi kwa mlalamikaji na mlalamikiwa, migogoro kumalizwa kwa maridhiano na kutatuliwa kwa muda mfupi.

Awali akifungua mafunzo hayo, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la KWIECO, Peter Mashingia, alisema wanatamani kuona wajumbe hao wa mabaraza wanachaangia kuwapo kwa ongezeko la utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia mfumo wa ADR kwa ufanisi.

Alisema: “Maana yake ni kwamba kama takwimu za mwaka jana mlikuwa mmefikia watu 100, tunatamani kuona wale ambao wana ile migogoro inatatuliwa kwa haraka katika hizo siku 30. Na hilo ongezeko lake linaonekana kwa takwimu ambazo ziko ndaani ya kata”.

# Washauri kuanzishwa sheria kali dhidi wauzaji tiba asili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa mradi wa afya yangu, mtaji wangu, unaohamasisha matumizi ya huduma mkoba za chanjo ya ugonjwa wa UVIKO-19 katika Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wameishauri serikali kuja na sheria kali ya kuzuia tiba asili ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kisayansi.

Wamesema kwa kufanya hivyo watakuwa wamelinda afya za Watanzania wanaokimbilia huduma hizo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika Mji wa Moshi, wakati wa kikao kazi cha kuhitimisha mradi huo kilichoandaliwa na Shirika la TUSONGE CDO, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Susan Lawi, alisema baadhi ya tiba asili zinatumika vibaya bila kujali afya ya mtumiaji na hazijafanyiwa vipimo vya kisayansi.

“Kuzuka tu kwa tiba asili ambazo hazijafanyiwa utafiti kuna athari kubwa kwa jamii na taifa kwa ujumla. Lazima Wizara ya Afya ijiridhishe na hili. Aidha, kuna mambo pia kama kuzagaa kwa taarifa ambazo siyo sahihi kuhusu chanjo. Kumeathiri huduma za chanjo,” alisema.

Aidha, Linda Macha kutoka JWWUK, aliishauri serikali kutumia mashirika ya kiraia linapojitokeza janga lolote au mlipuko wa magonjwa katika kutoa elimu kwa umma.

Naye dereva bodaboda, Godgrant Mmari, mkazi wa Ivaeny, Wilaya ya Siha, alisema kundi hilo liliguswa na mradi huo moja kwa moja na kupata elimu sahihi na kisha kupata chanjo ya UVIKO-19.

Mratibu wa mradi huo, Lawi Msemwa, alisema mradi huo ulijikita katika malengo makuu manne, ambayo ni kuendelea kutoa elimu kwenye jamii kufahamu nini maana ya UVIKO-19, kujikinga, athari zake na namna ambavyo ugonjwa huo huambukizwa.

Kwa mujibu wa Lawi, lengo la pili ni kuzijengea uwezo kamati za afya za msingi zilizoko ngazi ya vijiji, kuhakikisha kamati hizo zinakuwa na nguvu ya kutoa elimu.

Alisema lengo la tatu ni kuunga mkono kampeni ya kitaifa ya chanjo salama, ambayo kampeni yake inafanywa na serikali, lengo la nne ni kuunga mkono uhamasishaji wa utoaji wa chanjo kwa njia ya huduma mkoba.

“Tulianza mradi huu Julai mwaka jana na tunategemea kuhitimisha mradi huu Juni mwaka 2023. Wanajamii tuliowagusa na kuanza nao ni watoa maamuzi kwenye ngazi ya jamii, wakiwamo viongozi wa vitongoji, serikali za mitaa, kata; kwa kujua kwamba ndiyo wenye mamlaka ya kukutana na wanajamii moja kwa moja. “Tuliwagusa pia, walioko kwenye maeneo hatarishi kama kundi la waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda. Kundi hili ni linakaa maeneo ya wazi na wanabeba abiria wa aina mbalimbali na wao ni rahisi sana kupata maambukizi.

“Wamo vilevile wanafunzi wa vyuo vikuu, ambapo kwa Kilimanjaro, tuna vyuo kama Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini cha Sayansi ya Tiba na Uuguzi cha KCMC, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge (MWECAU), Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Stephano Moshi (SMUCo) na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).



Abiria wakisongwa na wafanyabiashara wadogo wakati wa kupanda basi katika stendi kuu ya mabasi wilayani Muheza mkoani Tanga, kitu ambacho ni kero kwa abiria. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TARI yahimiza ukaguzi wa mbegu za ngano, shahiri

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIHA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI), imewahimiza wadau na wakulima wa ngano na shahiri katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, kuhakikisha mbegu wanazoingiza kutoka nje ya nchi zinapitia katika mamlaka za mazao mipakani.

Imesema hatua hiyo itadhibiti hatari ya kuingiza magonjwa ya mazao hapa nchini.

Wito huo umetolewa na Mtaalamu Mwandamizi wa Magonjwa ya Ngano na Shayiri, Salome Munisi, wakati wa kuhitimisha ziara ya siku nane wilayani Siha.

Alisema madaktari wa magonjwa kutu ya majani na mabua ya ngano, kutoka Kituo cha Kimataifa cha Kuboresha Mahindi na Ngano (CIMMYT) nchini Mexico wamefanya utafiti katika mikoa nchini baada ya ugonjwa wa BLAST kuingia Zambia.


“Tunaomba TARI na wadau, wakulima wa ngano na shayiri kujiepusha na kuingiza mazao ya nje ya nchi ovyo, ili tujiepushe kuleta ugonjwa huu na tumelazimika kufanya utafiti kwa nchi nzima kwa kushirikiana na wataalamu wabobezi wa mazao ya ngano duniani, ili kudhibiti ugonjwa huo usiingie Tanzania.

“Kwa kweli watafiti hawa wamekuja wakati muafaka, kwa ajili ya kuchunguza mwenendo wa magonjwa ya ngano, pamoja na kuchukua sampuli za magonjwa hayo, ili kupima kama kuna magonjwa mengine kama ugonjwa wa BLAST,” alisema Salome.

Kwa mujibu wa Salome, tahadhari zaidi inatakiwa kuchukuliwa na endapo mfanyabiashara au mkulima anataka kuingiza mazao nchini ni muhimu kupitia vyombo husika ili kukinga magonjwa hayo yasiathiri sekta ya kilimo hususani ngano na shayiri.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Siha, Regan Zablon, alisema ugonjwa unaosumbua zaidi wakulima wa wilaya hiyo kwa miaka mingi ni ugonjwa wa kutu ya majani na mabua, hivyo walishukuru wataalamu hao kufika kwa ajili ya kutafiti.

Watafiti wabobezi wa CIMMYT kutoka nchini Kenya, Dk. Sridhar Bhavan na Mexico, Dk. Hordson David, wa mazao ya ngano na mahindi, walisema ipo haja ya kila mdau kutumia mbegu bora ili kusaidia kuzalisha mazao bora ya ngano yenye mavuno mengi na inayostahimili magonjwa.



# Wazazi wakumbushwa kudhibiti matumizi teknolojia kwa watoto

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI mbalimbali katika mikoa ya Kanda ya Ziwa wameikumbusha jamii pamoja na wazazi kuzingatia malezi bora kwa watoto na kuweka udhibiti katika matumizi ya teknolojia lengo likiwa ni kudhibiti mmomonyoko wa maadili.

Walitoa wito huo kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki kufuatia maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyoadhimishwa katika maeneo mbalimbali yakiwa na kauli mbiu ya 'zingatia usalama wa mtoto katika ulimwengu wa kidijitali'.

Akizungumza katika maadhimisho hayo Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, alisema katika ulimwengu wa kidijitali wazazi wanapaswa watumie vizuri teknolojia kwa maendeleo endelevu na siyo kusahau malezi ya watoto na kutumia muda mrefu katika mitandao. Alisema hali hiyo husababisha mmomonyoko wa maadili.

Naye Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema serikali itaendelea kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili, pamoja na kuunda mabaraza ya watoto ambayo husaidia kupasa sauti za vitendo vya ukatili.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe alipiga marufuku tabia za baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto walemavu ambao wamekuwa wakisaidiwa vifaa kwa ajili ya watoto lakini wao wamekua wakivitumia kwa matumizi tofauti kuacha tabia hiyo mara moja.

"Wadau mbalimbali wanajitoa kuwasaidia watoto wenu likiwamo shirika hili la NELICO lililotoa viti mwendo 20 vyenye thamani ya Sh.milioni 40 vitakavyowasaidia watoto wenu oleweni mviuze tutaelewana, tumieni kwa mstakabari wa maisha ya watoto hawa," alisisitiza

Mwenyekiti wa ashirika yasiyokuwa ya kiserikali mkoani Geita na Mkurugenz wa Shirika la NELCO, Paulina Alex Majogoro aliiomba jamii kushiriki katika kutoa ushahidi wa kesi za watoto mahakamani na kuzuia ukatili akisema ni wajibu wa kila mtu ili kukomesha ukatili wa watoto .

Aidha alieleza kuwa tofauti na msaada wa viti mwendo vilevile wametoa kadi za matibabu 50 kwa watoto wenye ulemavu kutoka Halmashauri ya Geita zilizo gharimu Sh.milioni 1.5 lengo likiwa ni kuwasaidia kupata matibu haraka pamoja na kompyuta 20 kwa shule za msingi 20.

Wakati huohuo wilayani Sengerema, Mkuu wa Wilaya hiyo, Senyi Ngaga alisema mzazi ama mlezi anao wajibu wa kulea na kumlinda mtoto yeyote kwenye jamii ili asipate matatizo, kumsaidia mtoto huyo kutimiza ndoto zake.

Alisema kuwa wananchi wanatakiwa kutoa taarifa za vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa watoto nyumbani na mitaani, lengo likiwa ni kupunguza wimbi la watoto wa mitaani na kuwa na taifa lenye watoto makini kwa maendeleo ya baadae.

Aidha takwimu za Jeshi la Polisi na kitengo cha ustawi wa jamii katika halmashauri hiyo kuanzia mwaka 2021 hadi 2023 zinaonyesha kuwa watoto 1,074 walifanyiwa ukatili wa aina mbalimbali kama vile vipigo, ulawiti, mimba za utotoni, kutelekezwa, pamoja na waliokosa matunzo hali inayosababisha matukio hayo kuzidi kuhatarisha maisha ya Watoto.

**Imeandaliwa na Alphonce Kabilondo (GEITA), Marco Maduhu, (SHINYANGA), Elizabeth Seleman (SENGEREMA)**

## Wakazi Shinyanga waitwa kupata vyeti vya kuzaliwa

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umewataka wakazi wa Shinyanga na maeneo jirani kujitokeza kwa wingi kujisajili na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa hususani katika kipindi hiki cha kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inayoendelea mkaoni humo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi katika Manispaa ya Shinyanga, Ofisa Habari wa RITA, Goodluck Malekela, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaendelea kuwahudumia wananchi wa mkoa huo pamoja na maeneo ya jirani.

"Ni vyema wakachangamkia fursa hii na kuja kwa wingi kusajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa kwani vyeti hivyo vina umuhimu mkubwa na vitawasaidia kwenye mambo mengi ikiwa ni pamoja na uombaji wa ajira, elimu hata kupata kitambulisho cha uraia,"alisema Malekela.

Alieleza kuwa wananchi mbalimbali wameendelea kujitokeza kusajiliwa na kuchukua vyeti vyao huku wakiiomba serikali kuendeleza utaratibu wa kufanya kampeni za namna hiyo mara kwa mara lengo likiwa ni kuwafikishia huduma karibu.

Mkazi wa Old Shinyanga, Shija Kulwa alisema serikali imefanya jambo jema kuanzisha zoezi hilo ambalo litawawezesha watu wengi kupata vyeti vya kuzaliwa.

RITA imeweka kambi ya siku 10 mkoani Shinyanga kwenye viwanja vya Sabasaba Manispaa ya Shinyanga kuanzia Juni 11, 2023 hadi 20 Juni 2023.

Lengo kuu ni kuendelea kutoa huduma ya usajili wa vyeti vya kuzaliwa na kutoa elimu juu ya mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia.



Madereva bodaboda wa Tarafa ya Sirari mkoani Mara wakisafirisha mahindi ya wafanyabiashara yaliyozuiwa mpakani mwa Tanzania kuingia nchini Kenya kwa ajili ya kuuza. **PICHA: SAMSON CHACHA**

# H/shauri Biharamulo yapewa 5 ripoti CAG

**Na Daniel Limbe,** BIHARAMULO

MKAGUZI Mkuu wa Nje wa Hesabu za Serikali mkoani Kagera, Godwin Ibrahimu, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo mkoani humo kwa kupata hati za safi katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Alitoa pongezi hizo juzi katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, kilichoketi kwa lengo ya kujadili hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2021/22.

Alieleza kuwa hali ya halmashauri hiyo kuwa na hati safi katika hoja zote za CAG ni hatua nzuri inayoonyesha uadilifu na umakini katika kusimamia fedha za serikali na utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Akitoa salamu za Mkuu wa Mkoa wa Kagera katika kikao hicho, Katibu Tawala wa mkoa huo, Toba Nguvila alisema ili kufikia malengo yanayokusudiwa na serikali madiwani wa halmashauri hiyo hawana budi kuwa wakali.

Alisema zipo taarifa za baadhi ya watumishi waliotafuna fedha za michango ya wananchi na bado hatua za kisheria hazijachukuliwa, huku akiiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi wa haraka ili itakapo thibitika wahusika wachukuliwe hatua za haraka.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Leo Rushahu, aliwataka viongozi wote kuendeleza ushirikiano mzuri uliopo kati ya madiwani na watumishi, lengo likiwa ni kuhakikisha wilaya hiyo inaendelea kupiga hatua kubwa za maendeleo ikiwa ni pamoja na kusimamia vyema fedha za umma.

Nipashe
Spotika



MBAPPE, KANE AU HAALAND NANI ANAYEFAA MADRID UK. 12-13



KHEPHREN THURAM

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ousmane Dembele, amesema anaamini wapinzani wao Real Madrid watakuwa dhaifu baada ya kuondoka ghafla kwa Karim Benzema. Benzema, mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or aliamua kuachana na Real Madrid na kutimkia Saudi Arabia kujiunga na klabu ya Al Ittiahad inayoshiriki ligi ya 'Saudi Pro League'. Dembele alisema bila Benzema, Real Madrid haitakuwa sawa kwa sababu yeye ndiye anayeshikilia Ballon d'Or na mchezaji mkubwa.



# VIUNGO 6 WANAOWEZA KUFITI LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

DIRISHA la usajili la Liverpool majira ya joto limeanza vyema hasa baada ya kumnasa mshindi wa Kombe la Dunia, Alexis Mac Allister kutoka Brighton & Albion.

Ujio wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 unachukuliwa kuwa kazi kubwa sana, huku Mac Allister akiwa msingi wa Brighton kumaliza katika nafasi sita za juu kwenye Ligi Kuu England ambayo imeimarisha nafasi ya kushiriki Ligi ya Europa msimu ujao.

Lakini badala ya kujiunga na Albion katika mradi wao mpya, Mac Allister atacheza katika mashindano hayo na Liverpool, akiwa na jukumu la kusaidia kufufua safu ya kiungo ambayo ilizidiwa mara nyingi mwaka jana.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ameidhinisha kuachiwa kwa Naby Keita na Alex Oxlade-Chamberlain kwa uhamisho wa bure - wakati James Milner anaonekana kuelekea Brighton baada ya mkataba wake kumalizika - hivyo hii inaweza kuwa majira ya mpito kwa Wekundu hao wakati wanatafuta kuanzisha maisha mapya.

Hapa tunawaangalia viungo sita wanaoweza kufiti Liverpool.

### #1. Manu Kone

90minutes ilifichua mwishoni mwa Mei kwamba, Liverpool walikuwa wameanza mazungumzo na wawakilishi wa kiungo wa kati Mfaransa, Manu Kone baada ya msimu mzuri sana kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 anacheza nafasi ya kiungo wa kati na ni mtu ambaye Schmadtke anamfahamu vyema tangu alipokuwa Ujerumani. Mrithi anayetarajiwa wa muda mrefu wa Fabinho, ambaye alitatizika msimu mzima uliopita, dili la Kone linaweza lisivunje benki pia jambo ambalo Liverpool wanatazamia katika usajili wao wa majira ya joto.

### #2. Khephren Thuram

Kiungo anayependa ushambulizi zaidi, Khephren Thuram ni mchezaji mwingine ambaye Liverpool wamefanya mazungumzo juu ya uwezekano wa kuhamia Anfield.

Thuram, ambaye ni sehemu ya kikosi cha Ufaransa cha Didier Deschamps kwa ajili ya mechi zijazo za kimataifa, ni mtayarishaji wa nafasi ambaye daima anatazamia kuendeleza mpira mbele katika maeneo ya juu kama ilivyo kwa Mac Allister.

### #3. Ryan Gravenberch

Ryan Gravenberch alitangazwa kuwa mmoja wa vijana mahiri katika soka la Ulaya alipobadilishana Amsterdam na kwenda Munich majira ya joto yaliyopita.

Lakini kushindwa kuwaondoa Joshua Kimmich na Leon Goretzka kutoka majukumu yao ya kuanzia, pamoja na kuongeza Konrad Laimer kwa msimu ujao, kunamaanisha Gravenberch anaweza kupatikana baada ya miezi 12 migumu kwake.

Kiungo mwingine anayependa mashambulizi zaidi, Gravenberch hutengeneza nafasi lakini pia anapenda kutumia juhudi langoni.

### #4. Youri Tielemans

Ikiwa ni uzoefu wa Ligi Kuu ya England ambao Liverpool wanatafuta, hawapaswi kuangalia zaidi ya Youri Tielemans.

Sio tu kwamba Mbelgiji huyo anajua njia yake ya kuzunguka kitengo hicho, pia atakuwa mchezaji huru msimu huu wa joto kwani mkataba wake wa Leicester City unamalizika na amechagua kutoongeza tena - haishangazi kwa sababu Mbweha hao wameshuka daraja.

Tielemans alikuwa chini ya kiwango chake bora wakati wa 2022/23 lakini ana ubora halisi anaweza kuwa nyongeza bora zaidi.

### #5. Gabri Veiga

Gabri Veiga ni mchezaji mchanga mwenye kipaji wa Hispania ambaye anaweza kuwa nyota halisi katika siku zijazo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ana takribani klabu zote bora zaidi barani Ulaya zinafuatilia maendeleo yake na atakuwa amefanya nafasi yake ya kuchukua hatua isiyokuwa na madhara baada ya kuifungia Celta mabao mawili katika ushindi wao wa 2-1 dhidi ya Barcelona.

Magoli yake 15 yanaonesha kile anachoweza kufanya katika suala la matokeo, huku rufani yake ikiimarishwa zaidi na kifungu cha kuachiliwa cha pauni milioni 35 kilichoandikwa kwenye mkataba wake.

### #6. Ruben Neves

Baada ya misimu sita pale kwenye uwanja wa Molineux, wakati wa Ruben Neves kupata uhamisho mkubwa bila shaka ni sasa.

Hakuna aliyetarajia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kuwa Wolves kwa muda mrefu kama amekuwa, ukweli usemwe na maonesho yake katika 2022/23 yalikuwa ukumbusho kwamba Mreno huyo ana uwezo wa kuchanganya kiwango cha juu.

### Chaguzi nyingine

Kuna chaguo zaidi kwa Liverpool msimu huu wa joto ikiwa wako tayari kulipa fedha nyingi, huku mtandao wao mkubwa wa skauti ukithamini vipaji vya Moises Caicedo na Aurelien Tchouameni miongoni mwa wengine.

Nicolo Barella, Romeo Lavia na Mason Mount wote wana mashabiki wanaovutiwa huko Anfield pia, na watatu hawa wanaweza kutoa kifuniko katika nafasi ya sita, nane na kumi.




# MBAPPE, KANE AU HAALAND NANI ANAYEFAA REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

DIRISHA la uhamisho wa majira ya joto si la kufurahisha bila jasho na hofu kwamba Real Madrid itamsajili mchezaji wako bora.

**Sawa, 'furaha' huenda lisiwe neno sahihi katika mfano huo, lakini wakati Los Blancos hao wanawinda Galactico nyingine, ulimwengu wa soka ni mahali pa kuvutia zaidi.**

Inamaanisha, wote tunapenda sehemu ndogo za ukurasa wa mbele wa gazeti la Marca, siyo? Kila mtu ni kwa Sergio Ramos au nguli mwingine wa klabu akisisitiza kuwa mchezaji ana 'DNA ya Real Madrid'.

Karibu popote pale, Real Madrid wako sokoni kutafuta mshambuliaji.

Kuondoka ghafla kwa Karim Benzema kwenda Saudi Arabia kumemshangaza kila mtu, na uhamisho wa nyota wa zamani wa Stoke City, Joselu hauwezi kuwa pekee ambao miamba hao wa Hispania wamefanikiwa msimu huu wa joto.

90minutes inaelewa kuwa Real Madrid wanamtaka Kylian Mbappe wanayemlenga kwa muda mrefu, ambaye anaweza kuuzwa na PSG msimu huu wa joto baada ya kukataa kusaini mkataba mpya.

Harry Kane amebakiwa na mwaka mmoja kumaliza mkataba wake binafsi na Tottenham Hotspur na anaongoza kwenye orodha fupi ya Los Blancos ya washambuliaji asilia wa kati. Mchezaji wa Manchester City, Erling Haaland pia amekuwa akihusishwa na kuhamia Santiago Bernabeu.

Makala haya tunaangalia nani kati ya wachezaji hao watatu ambaye anafaa kwenye mfumo wa Real Madrid.

### BEI

Iwapo rais wa Real Madrid, Florentino Perez anafikiri kuwa anaweza kuingia PSG, Tottenham au Manchester City na kuondoka na wachezaji wao bora, hilo liko wazi kabisa.

Habari njema ni kwamba, PSG wanaonekana kukubali kumpoteza nyota wao wa mbele - wanashikilia kuwa hataondoka bure msimu ujao wa joto na kwa hiyo mazungumzo yanapaswa kuwa rahisi kinadharia.

Spurs, hata hivyo, bado wana matumaini kuwa Kane anaweza kusaini mkataba mpya (kwa sababu yoyote ile) na wanaonekana kana kwamba mkataba wake unaisha 2034 badala ya 2024.

Kwa hakika Haaland yuko nje ya meza msimu huu wa joto na Real Madrid labda wanapaswa kuangalia sehemu nyingine.

### ANAYEFITI

Ikiwa Real Madrid wanataka mbadala wa Benzema, basi Kane ndiye njia ya wazi.

Nahodha huyo wa England ni mfungaji mabao mzuri na anayeweza pia kusaidia. Anaweza kushuka chini kuwatengenezea wachezaji wenzake uwepesi. Vinicius Junior kimsingi ni ni kama Son Heung-min. Ni ushirikiano ambao unaweza kuigwa kwa urahisi nchini Hispania.

Tatizo la Mbappe ni kwamba anacheza nafasi na sawa na Vinicius. Wakati Real Madrid hawana wasiwasi juu ya kumchezesha Mfaransa huyo katikati, ni shida ambayo imekuwa ikiisumbua PSG katika misimu michache iliyopita.

Mbappe inasemekana aliiomba PSG kusajili mshambuliaji wa asili wa kucheza katikati hapo awali na amecheza kama namba tisa bila kupenda, akipendelea kuingia kutoka winga ya kushoto.

Kane na Mbappe wote wanaweza kujivunia safu tofauti kwenye safu zao za ushambuliaji, lakini inaweza kuwa ngumu zaidi kwa Real Madrid kujumuisha mfungaji bora Haaland kama vile anavyochezeshwa na Pep Guardiola akiwa Manchester City.

### USTAA

Timu nyingi zingezingatia (na hazipaswi) kuzingatia hili, lakini hii ni Klabu ya Real Madrid tunayoizungumzia hapa.

Kuna mshindi wa wazi katika kitengo hiki, pia. Mbappe anatoa haiba ndani na nje ya uwanja. Anauzwa sana kwa mtu ambaye amecheza maisha yake yote katika Ligue 1 na anaweza kuinua hadhi yake hadi kiwango cha hadithi kwa kuhamia mji mkuu wa Hispania.

Haaland amegeuka kuwa mtu bora zaidi tangu ajiunge na Manchester City ingawa anabakia kuwa sio maarufu sana nje ya uwanjani, lakini Kane pia yupo kwenye wakati mzuri kwenye kitengo hicho.

Ingawa Mbappe na Kane wanaweza kuwa maarufu zaidi kushinda Halaand.

Hivyo kwa mantiki hiyo, Mbappe na Kane ndio wanaofiti hapa.

### KAULI

Huenda hiki ndio kipengele kilicho karibu zaidi, au angalau Mbappe ingawa sio mshindi dhahiri.

Ni wazi kwamba, hatima kwa Mfaransa huyo ni kuvaa jezi ya Real Madrid siku moja, hata kama si mara moja.

Lakini kuchukua nyota mwingine kutoka kwa mikono ya Daniel Levy? Je, unaenda kwenye nyumba ya washindi watatu na kuchukua mchezaji wao bora baada ya kupoteza 4-0 huko mwezi mmoja uliopita? Hiyo itathibitisha Real Madrid bado wako kileleni mwa sehemu ambayo nyota wengi wangepeda kwenye kucheza.

### HITIMISHO

Mshangao wa kushangaza, uamuzi ni kwamba Real Madrid wanapaswa kujitosa kwa Mbappe.

Inaleta maana zaidi, si lazima kunawahitaji kuvunja benki na kuendana na nyakati za timu yao changa, inayokuja inayoongozwa na Vinicius na Jude Bellingham.


Ongezeko la Mbappe kwenye mchanganyiko huo na Real Madrid utaifanya kuwa timu bora zaidi kuliko ile iliyokuwa na wakati mgumu kwa msimu wa 2022/23.

## Nukuu

"Kwanza kabisa, Xavi alikuwa mchezaji bora na ninaiheshimu sana Barcelona, Lakini sielewi kwa nini 'wanataniana' na mchezaji wetu kwa uwazi na kwa kukera. Joshua Kimmich ni jiwe kuu la msingi kwetu, hatuwezi kumuuza na bado ana mkataba na sisi (Bayern Munich)." **Rais wa Bayern Munich, Herbert Hainer akizungumzia tetesi za nyota wa timu hiyo Kimmich kutakiwa na mabingwa wa Hispania, Barcelona.**




"Sina maswali kichwani anaweza kufanya hivyo, tulizungumza kuhusu hilo wiki nne zilizopita kwenye simu na amefurahishwa na hilo, alionyesha kile tunachofikiria anaweza kukiweza na anatupa kitu tofauti na viungo wetu wengine, bila shaka, mengi yatakayotokea yatategemea klabu yake. Ukweli ni kwamba amekuwa akicheza kwa kiasi fulani ndani na mpira umesaidia mabadiliko yake." **Kocha wa timu ya taifa ya England akimzungumzia mchezaji wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold.**



"Nafurahi sana kuona nimeisaidia timu yangu kupata pointi, matokeo haya ni muhimu sana kwetu, ni kazi ya wachezaji wote pamoja na benchi letu la ufundi, tunaangalia mbele kuhakikisha tunafuzu kwa fainali za Ulaya, nina uhakika tunaweza kufanya hivyo," **Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, akizungumzia matokeo ya mchezo wao dhidi ya Austria.**



# 'THANK YOU' SIMBA, YANGA, AZAM ZILIVYOTIKISA




**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni wiki ya aina yake kwa mashabiki wa soka nchini, wakati klabu kubwa nchini, Simba, Yanga na Azam FC zilipokuwa zikitoa mkono wa kwa heri kwa wachezaji, makocha na watu wa mabenchi ya ufundi.

Ni kama zilikuwa zinashindana hivi kutoa taarifa hizo kwenye mitandao yao ya 'Instagram'. Huyu akitoa hii na mwingine anatoa ya kwake.

Wakati mwingine sasa ikawa kama burudani hivi kwa mashabiki wa wasomaji, na kama kawaida ya Watanzania, utani ukawa mwingi kwenye mitandao ya kijamii.

Neno lililokuwa likitumiwa zaidi kama kichwa cha habari ni la kiingereza 'Thank you' na baada ya hapo inafuata taarifa ya kuachana na wanaowaacha.

Simba na Azam ndiyo zilizotia fora kwa kuagana na wafanyakazi ke wake wengi, tofauti na Yanga ambapo wao wameachana na wawili tu.

Simba yenyewe ilitia fora kwa kuchapisha 'thank you' kila baada ya muda mfupi kwa siku moja, tofauti na Azam ambayo angalau ilikuwa ikifanya hivyo kila baada ya siku moja.

Neno 'thank you' likaanza kuwa maarufu kwa mashabiki wa soka ambao kwa sasa wameanza 'kumiss' soka baada ya msimu wa mashindano kumalizika. Burudani yao sasa ikawa ni kwenye mitandao ya kijamii kujadili posti hizo.

Na utani mwingi ukaendelea, wengine wakaenda mbali kuwa mwisho wanaweza kuona posti za 'thank you' kwa wachezaji, makocha na viongozi ambao ndiyo muhimili wa klabu zenyewe. Huo ni utani tu.

Lakini kwa mujibu wa viongozi wa klabu hiyo, lengo ni kuondoa baadhi ya watu na kuleta wengine kwa ajili ya maboresho wa timu zao kwa msimu ujao wa ligi.

Ni Yanga tu ndiyo makocha wao wameondoka kwa sababu ya kumaliza mikataba, huku wao wakitaka kuwaongeza, lakini ikashindikana.

Mwandishi wa makala haya amekusanya taarifa za wachezaji, makocha walioondoka au kuachwa na klabu hiyo.

**1. Nasreddine Nabi-Yanga**

Yanga ilikuwa inamhitaji sana kocha huyu aendelee kubaki na sababu zinaeleweka kwa kila mtu kwani ndiye kinara wa mafanikio ya misimu miwili mfululizo, hasa huu.

Viongozi wa klabu hiyo walijitahidi kutaka kumbakisha, lakini baada ya mazungumzo marefu ilishindikana.

Nabi ameondoka Yanga na taarifa zinasema klabu ambayo huenda akatua ni Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, na huenda akaondoka na robo tatu ya benchi lake ya ufundi.

**2. Chlouha Zakaria-Simba**

'Thank you' za Simba ilianza kwa kocha wa magolikipa, Chlouha Zakaria raia wa Morocco. Alijiunga na Simba Novemba mwaka jana, lakini ni mmoja wa watu walioachwa ili kupisha maboresho.

**3. Bruce Kangwa-Azam FC**

Mpaka sasa ni Azam pekee ambayo 'thank you' zake zimelenga mpaka kwa wachezaji. Zimemgusa nahodha wa klabu hiyo Mzimbabwe Bruce Kangwa ambaye amepewa mkono wa kwa heri. Alisajiliwa na timu hiyo mwaka 2016 akitokea nchini Zimbabwe.

**4. Kelvin Mandla-Simba**

Huyu ni kocha wa viungo wa klabu ya Simba raia wa Afrika Kusini. Naye alijiunga Novemba mwaka jana kwa mkataba wa mwaka mmoja. hata hivyo ni mmoja wa walioachwa msimu huu, akipigiwa kelele na wanachama na mashabiki wengi kuwa ameshindwa kuwafanya wachezaji kuwa na stamina na pumzi.

**5. Milton Nienov - Yanga**

'Thank you' nyingine kati ya nyingi wiki hii, ilikwenda kwa kocha wa magolikipa wa Yanga ambaye yeye amemaliza mkataba wake kwenye klabu hiyo. Awali alifanya kazi kwenye klabu ya Simba.

**6. Kenneth Muguna - Azam FC**

Ni kiungo mkabaji raia wa Kenya, ambaye Azam imeamua kuachana naye na kumwambia 'thank you', kwa kazi nzuri aliyoifanya huko nyuma.

Alisajiliwa 2021 akitokea klabu ya Gor Mahia ya Kenya, hivyo hatokuwa sehemu ya timu hiyo msimu ujao.

**7. Fareed Cassim-Simba**

Ni mtaalam wa viungo na misuli wa klabu hiyo ambaye ni Simba wameamua kuachana naye, sababu kuwa ikiwa ni kuumia mara kwa mara kwa wachezaji, lakini pia wanachelewa kupona, hivyo sehemu hiyo ni moja kati ya sehemu ambazo Simba wanataka kuboresha. Alishawahi kufanya kazi Yanga.

**8. Rodgers Kola-Azam FC**

Straika huyu raia wa Zambia naye amepewa mkono wa kwa heri, akiwa amejiunga na klabu ya Azam FC 2021, akitokea Zanaco ya nchini humo.

**9. Cleophace Mkandala-Azam FC**

Kiungo huyo alisajiliwa na Azam mwaka jana, ikiipiku Simba katika kinyang'anyiro cha kumuwania kutoka Dodoma Jiji, lakini leo hii ni mmoja wa wachezaji waliopewa 'thank you', ili kupisha wengine kuendeleza jahazi.

**10. Ismail Aziz Kada-Azam FC**

Azam FC ilimsajili winga huyu kutoka Prisons mwaka 2020 akiwa kwenye kiwango cha juu na aliisaidia kwenye mechi za msimu uliopita. Msimu huu yupo kwenye orodha ya walioonyesha mlango wa kutokea.

**11. Kalimangonga Ongalla-Azam FC**

Pamoja na kucheza mechi 32, akiongoza kushinda 21, sare nne na kupoteza saba, lakini Azam FC imeona haitoshi, ikampa mkono wa kwa heri, kocha wake na mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Kalimangonga Ongalla.

**12. Aggrey Morris-Azam FC**

Azam ikaendelea kushangaza wengi ilipompa 'thank you' nahodha wake wa miaka mingi, Aggrey Morris ambaye hadi wanaachana naye alikuwa kocha msaidizi wa timu hiyo.

**13. Wibol Maseke-Azam FC**

Kwa kuonyesha kuwa imedhamiria kusafisha, Azam FC imempa mkono wa kwa heri mchezaji ambaye ilimlea yenyewe kwenye kituo chake cha kukuza vipaji na kumpandisha msimu wa 2019, Wibol Maseke. Sasa yupo huru kwenda timu yoyote ile.

**JE, WAJUA?**

FIFA the Good of the Game

RIPOTI iliyotolewa na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) inasema kulikuwa na machapisho ya matusi na lugha za ubaguzi zaidi ya 20,000 yaliyowalenga wachezaji, makocha na viongozi wakati wa Kombe la Dunia mwaka jana. Ongezeko kubwa la unyanyasaji na ubaguzi kwenye fainali hizi lilikuja baada ya England kupoteza mchezo wa robo fainali dhidi ya Ufaransa, Harry Kane alipokosa mkwaju wa penalti dakika za lala salama.



# Chongolo aiagiza NARCO kuwawezesha wafugaji

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameiagiza Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuwawezesha wafugaji wadogo wafuge kisasa na kuondokana na ufugaji wa kienyeji ambao hauna tija kwao.

Alitoa agizo hilo juzi alipotembelea Ranchi ya Kongwa mkoani Dodoma ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM katika majimbo yote ya mkoa huo. Alisema kuna wafugaji ambao wana mifugo mingi lakini haiwafaidishi kutokana na kukosa elimu ya ufugaji kisasa na kibiashara.

Chongolo alisema aliwahi kukaa katika Wilaya ya Longido kwa wafugaji na kukuta mfugaji ana ng'ombe 1,000 lakini analalia ngozi, hafanani na mali anazomiliki.

Aliwataka wafugaji kubadilika kutoka kuwa waswaga makundi ya ng'ombe na mifugo mingine hadi kuwa mabilionea kutokana na uwingi wa mifugo wanayomiliki.

Pia aliwaagiza wafugaji hao kupelekewa mbegu za majani ya mifugo kwa ajili ya malisho ya wanyama hao wa kawaida hasa katika kipindi cha msimu wa kiangazi ambacho kuna tatizo la malisho.

Aidha, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi bado ipo nyuma katika kutoa elimu ya kuwawezesha wafugaji wa kawaida kufuga kibiashara kutokana na kuwa na wanafugaji ambao wanafuga kienyeji.

Awali, Mkurugenzi wa NARCO, Prof. Peter Msofe alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023 walipewa bajeti ya Sh. bilioni 4.6 ambazo zilitumika kununua mbegu bora ya ng'ombe na kununua mashine za kuvunia majani ya mifugo.

Hivyo aliiomba serikali kuwawezesha Sh. bilioni 74 kwa lengo la kununua ng'ombe 10,000 na ambao watanenepeshwa na kuuza nyama kwenye maduka yalipo maeneo ya mjini.



Makamu wa kwanza wa Rais na Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, akizungumza na wananchi katika Kijiji cha Chinagali wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

# Wakulima wa alizeti waomba mikopo ya riba nafuu

**Na Joseph Mwendapole,**
DODOMA

WAKULIMA wa alizeti mkoani Dodoma wameziomba taasisi za fedha nchini kuwapa mikopo ya riba nafuu ili kuzalisha zao hilo kwa wingi, kuisaidia nchi kuondokana na utegemezi wa mafuta ya kupikia nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Eso Oil Company ya Kibaigwa mkoani humo, Evalyne Thompson, alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu namna Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo nchini (AMDT), ilivyosaidia kuinua zao hilo kwa wakulima nchini.

Alisema wakulima wakiwezeshwa kwa kupewa mikopo isiyoumiza wana uwezo mkubwa wa kuisaidia nchi kwa kulima mashamba makubwa ya alizeti na nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kupikia.

"Pamoja na kulima tuna matatizo yetu, kubwa ni mitaji ya kuboresha kilimo chetu. Kwa hiyo serikali au taasisi za fedha zikinisaidia mikopo nafuu nitaweza kulima mashamba makubwa na kuwalimia wakulima kisha kununua mazao yao kwa wingi, mimi nikaongeza kipato na wao wakaongeza kipato chao," alisema.

Aidha, alisema awali kiwanda chake kilikuwa kikikamua magunia 80 ya alizeti kwa siku lakini baada ya kuwezeshwa na Taasisi ya Kilimo ya Agricultural Development Denmark Asia (ADDA) kwa kuongezewa mashine ya kukamua sasa anaweza kukamua hadi magunia 200 kwa siku moja. Alisema kero kubwa wanayopata kwenye shughuli zao za kila siku ni ukosefu wa umeme wa uhakika kwani eneo hilo lina viwanda vingi vidogo lakini vinashindwa kufanyakazi kutokana na kukaa muda mrefu bila kuwa na umeme.

Mmoja wa wakulima, Khadija Iddi ambaye ni mmiliki wa kiwanda cha Nyarega Sunflower Oil Kibaigwa, alisema iwapo watawezeshwa kwa mikopo watatanua shughuli zao na kuchangia upatikanaji wa mafuta maeneo mengi nchini. Alisema watu wa ADDA walimwezesha kuongeza mashine ya kukamulia alizeti ambayo kwa kiwango kikubwa imemwezesha kuboresha shughuli zake kwa kupata uwezo wa kukamua alizeti nyingi.

# RC aagiza madiwani kujadili hoja za CAG kila mwezi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameagiza Kamati ya Fedha na Uongozi kwenye mabaraza ya madiwani kuweka agenda moja ya kujadili hoja za ukaguzi zinazoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye halmashauri zao kila mwezi.

Akizungumza juzi kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ambacho kiliketi kwa ajili ya kujadili hoja za CAG za mwaka 2021/22, alisema kama kamati hizo zitajiwekea utaratibu huo kutamfanya Mkurugenzi wa Halmashauri na watendaji wake kutambua kuwa madiwani wanafuatilia kwa karibu mambo hayo.

"Tukiwa tunafanya hivyo tutajua mzembe anayetukwamisha ni nani na ikiwa mkuu wa idara ataonekana amekaa zaidi ya miezi sita bila kujibu hoja za CAG ambazo zinajitokeza katika idara yake tuandikieni barua kutujulisha," alisema Serukamba.

Alisema kimsingi kuwapo kwa hoja nyingi za CAG kwenye halmashauri ni suala la uzembe wa baadhi ya watendaji kutokuwa makini kufuatilia majukumu yao na kuagiza kila mtumishi ahakikishe anawajibika ipasavyo ili kila halmashauri kusiwe kunajitokeza hoja za CAG. Kuhusu suala la ukusanyaji mapato katika Halmashauri ya Wilaya Iramba alisema bado hali siyo nzuri hasa kutokana na baadhi ya watumishi kuendelea na tabia ya kula fedha mbichi wanazozikusanya badala ya kuzipeleka benki.

Hivyo, alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, kukomesha vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wenye tabia ya kufuja fedha walizozikusanya.

Naye, Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema madiwani wahakikishe hoja za ukaguzi za CAG hazijirudii mara kwa mara kila mwaka kwa kuwa hali kama hiyo ikiwa inajitokeza itasababisha halmashauri kupata hati mbaya.

Aliwapongeza madiwani na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa jitihada kubwa walizozifanya na kupunguza hoja za CAG kutoka 113 na kubakia hoja 33.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Iramba, Michael Matomora, alimhakikishia mkuu huyo kuwa tabia ya ulaji wa fedha mbichi haitajirudia tena katika halmashauri hiyo na atachukua hatua kali kwa watumishi watakaobainika kufanya vitendo hivyo.



# Wananchi waiangukia serikali upatikanaji majisafi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Mji wa Chunya mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kutatua kero ya upatikanaji wa maji ya bomba inayoukabili mji huo.

Wamesema kuwa hali hiyo imekuwa ikiwasababishia gharama za maisha kuwa juu na kuwa katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Walitoa kilio hicho mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera uliokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi.

Wakazi hao walisema kutokana na tatizo hilo wanalazimika kununua maji kwa bei kubwa.

Mmoja wa wananchi hao, Safia Hamad alisema tatizo hilo linakuwa kubwa zaidi kipindi cha kiangazi ambapo maji huwa hayatoki kabisa kwenye mabomba.

Alisema serikali iliwapelekea mradi wa kuchimba visima virefu vya maji ambavyo hutumika kuvuta maji na kujaza kwenye matangi lakini kipindi cha kiangazi visima hivyo huwa vinakauka na hivyo kuwasababishia kukosa kabisa huduma hiyo.

"Tatizo hili ni kubwa kwa sababu kwa sasa maji huwa yanatoka mara moja kwa mwezi ama mara mbili, lakini watu wa Mamlaka ya Maji wanakuja kudai bili tunaomba serikali itusaidie," alisema Safia.

Zena Shabani ambaye ni mkazi wa Kitongoji cha Ujenzi katika Mji huo, alisema kipindi cha kiangazi huwa wananunua maji kwa vijana ambao huwa wanazungusha kwa kutumia maguta huku wakiwa hawana uhakika na usalama wa maji hayo.

Alisema wananunua ndoo moja ya lita 20 kwa Sh. 1,000 jambo ambalo alisema linawasababishia gharama za maisha kuwa juu kuliko uwezo wao wa kiuchumi.

Alisema wapo baadhi ya matajiri ambao wamechimba visima na wanawauzia lakini maji hayo yana magadi mengi kutokana na ardhi ya wilaya hiyo kuwa na madini mengi.

Diwani wa Kata ya Itewe, Alex Kinyama alikiri uwepo wa tatizo hilo na kwamba mradi wa visima haukufanya vizuri kutokana na miamba ya eneo hilo kuwa na mipasuko inayosababisha maji kupotea kwa kuzama chini.

Alisema Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya zitakazonufaika na mradi wa kupeleka maji kwenye miji 28 nchini na kwamba mradi huo ndiyo utakuwa suluhisho la tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Alisema wamepatiwa zaidi ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo huku akieleza kuwa wameanza kupata wasiwasi kutokana na mkandarasi aliyepata tenda ya kutekeleza mradi huo kutaka kubadili chanzo.

Alisema Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi pamoja na wataalamu wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) waliridhia chanzo cha maji cha Mto Gwaziva ambao upo umbali wa kilomita 30 kutoka kwenye mji huo ndicho kitumike.

"Kinachotushangaza ni kwamba mkandarasi aliyekuja tunaambiwa anachimba tena visima, mradi wa visima hapa kwetu hauwezekani kwa sababu ule wa awali ulishindikana kwa sababu ya aina ya miamba iliyopo hapa," alisema Kinyamagoha.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Chunya (CHUWASA), kuhakikisha wanatafuta suluhisho la muda mfupi wakati taratibu za utekelezaji wa mradi wa miji 28 zikiwa zinaendelea.

Vilevile alimtaka mkandarasi anayetekeleza mradi huo kwenda kuripoti kwenye ofisi yake ili apewe wataalamu watakaomshauri namna ya kutekeleza mradi huo vizuri.

Aliwataka viongozi wa serikali katika wilaya hiyo ya chunya pamoja na madiwani kuhakikisha wanashirikiana na mkandarasi huyo atakapoanza kazi ili mradi huo ukamilike mapema.



Wakazi wa Mji wa Chunya mkoani Mbeya wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera (hayupo pichani), mwishoni mwa wiki alipozungumza nao kwenye mkutano wa hadhara uliokuwa na lengo la kusikiliza kero. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wakulima Busokelo walia ucheleweshaji mbolea ruzuku

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAKULIMA wa Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wizara ya kilimo kuwawahishia mbolea ya ruzuku ili waendane na msimu wa kilimo.

Wakulima hao wanadai kuwa msimu uliopita pamoja na kwamba serikali iliweka ruzuku kwenye mbolea lakini bidhaa hiyo ilichelewa kuwafikia hali ambayo ilisababisha washindwe kuhudumia vizuri mazao yao.

Wakizungumza na Nipashe wakulima hao walisema katika maeneo mengi ya halmashauri hiyo gharama za usafirishaji wa mbolea kipindi cha mvua huwa zinakuwa kubwa.

Mmoja wa wakulima hao, Gwandumi Mwakatumbula, alisema katika eneo hilo msimu wa kilimo huwa unaanza mwishoni mwa Oktoba na hivyo wanaomba mbolea ziwafikie kabla ya muda huo.

Alisema msimu uliopita pamoja na mbolea kuuzwa kwa bei ya ruzuku lakini iliwafikia kuanzia Desemba hali ambayo umuhimu wake ulikuwa umekwisha.

"Nchi yetu misimu ya kilimo inatofautiana kati ya eneo moja na lingine, sisi tunaanza kupanda mahindi Oktoba, sasa ukituletea mbolea ya kupandia Desemba kama ilivyokuwa msimu uliopita unakuwa hutusaidii," alisema Mwakatumbula.

Naye Frola Sanga alisema katika maeneo hayo mbolea inatakiwa iwe inapatikana mwaka mzima kwa maelezo kuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi wanalima kilimo cha umwagiliaji hivyo wanahitaji mbolea muda wote.

Alisema yeye ni mkulima wa viazi mviringo na mahindi na kwamba anazalisha mazao hayo kwa kutegemea mvua na kwa kiasi kidogo anamwagilia kutokana na kutokuwa na uhakika wa uwepo wa pembejeo hizo.

# Chunya yaagizwa kutenga hekta 10,000 za wafugaji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeuagiza uongozi wa Wilaya ya Chunya kutenga eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 10,000 kwa ajili ya wafugaji ili kunusuru misitu ambayo inavamiwa na kufyekwa na wafugaji wanaohama kutafuta malisho na maji.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha baraza maalumu la madiwani cha kupitia na mujibu hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Homera alisema hali ya misitu katika wilaya hiyo ya Chunya ni mbaya hasa katika Kata ya Mafyeko na Kambikatoto ambazo zina wafugaji ambao wanavamia hata misitu ya serikali na kuweka makazi.

Alisema hali iliyopo katika maeneo hayo kuna uwezekano mkubwa miaka ya karibuni wilaya hiyo ikakabiliwa na tatizo la ukame utakaokuwa chanzo cha matatizo mengine ikiwamo ukosefu wa chakula.

Alisema eneo linalotakiwa kutengwa ni lazima liwe jirani na mto ili kuwarahisishia wafugaji hao kunywesha mifugo yao badala ya kusafiri kwenda kutafuta maji kwenye maeneo mengine hali ambayo huwa inasababisha migogoro mingine.

Alisema wakishatenga eneo hilo wanatakiwa kugawa vitalu ambavyo vitagawiwa kwa wafugaji hao na kuwapatia elimu ya namna ya kuvitumia kwa ajili ya mifugo.

"Mkuu wa wilaya kuna mambo mengi sana mazuri umeyafanya katika wilaya hii lakini hili la mifugo ndio mtihani wako uliobakia, hakikisha unalishughulikia kwa sababu kila tukiagiza mnasema Chunya hakuna eneo la kuchungia, hali ni mbaya sana ukipita eneo lile," alisema Homera.

Alisema kwa sasa hawezi kuruhusu operesheni ya aina yoyote kufanyika ya kuwaondoa wafugaji kwenye misitu kwa sababu hakuna eneo lililoandaliwa kwa ajili ya kuwapeleka.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Chunya, Noel Chiwanga alisema tatizo hilo kwa sasa lipo katika maeneo yote ya wilaya hiyo kutokana na wafugaji hao kuhama kutoka maeneo mbalimbali.

Alisema baadhi ya wafugaji wanavamia eneo la Kata ya Sangambi wakitokea katika Wilaya ya Mbarali na kwamba hali hiyo imetokana na operesheni zilizofanywa katika Bonde la Ihefu wilayani Mbarali. Vilevile alisema kuna maeneo mengine ya wilaya hiyo yaliyoko jirani na mpaka kati ya wilaya hiyo na Wilaya ya Songwe ambayo yamevamiwa na wafugaji hao.



# Watanzania wahimizwa kutumia mashine rafiki mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wamehimizwa kujikita katika matumizi ya bidhaa za viyoyozi ambavyo ni rafiki kwa mazingira.

Rai hiyo ilitolewa na Meneja wa Kampuni ya Garnet Star, Rajesh Nomulwar, wakati wa kusaini mkataba wa ushirikiano kati ya kampuni hiyo na Daikin.

Daikin ni mojawapo ya kampuni zinazoongoza kwa aina bora za viyoyozi duniani.

"Tumechagua kusaini mkataba wa kibiashara na Kampuni ya Daikin kwa kuwa ni moja ya kampuni ambazo zinaongoza kwa kuzalisha bidhaa ambazo ni rafiki kwa mazingira na ambazo zinahitajika kwa wingi sana hapa nchini Tanzania," alisema Rajesh.

Rajesh alisema moja ya sababu ya Kampuni ya Garnet kusaini mkataba huo ni ubunifu uliofanywa na Kampuni ya Daikin hivi karibuni pale ilipozalisha aina mpya ya viyoyozi ambazo ni rafiki kwa mazingira na ambazo zina nishati kidogo.

"Kwa upande wetu tuna mafundi wenye elimu ya kutosha katika kushughulikia bidhaa hizi mpya, ambao watazingatia ubora wa kimataifa wa Kampuni ya Daikin inayozalisha bidhaa hizo", alisema.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Daikin India, Toshiharu Tsurumaru na Meneja Mkuu wa Biashara za Nje wa kampuni hiyo, Jayant Jawa waliipongeza Kampuni ya Garnet Star kwa hatua iliyopelekea makubaliano hayo.

Wote waliahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Kampuni ya Garnet Star ili kuhakikisha Watanzania wanapata bidhaa zenye ubora sawa na thamani ya fedha watakazotumia wakati wa kuzinunua.

"Tuna furaha kubwa kuwa sehemu ya Tanzania kibiashara; tumekuwa tukipiga hatua katika kutekeleza majukumu yetu ya kibiashara katika ukanda huu wa Afrika kwa miaka kadhaa sasa", alisema.

Alisema kuwa Kampuni ya Daikin imelenga kuwa moja wapo ya kampuni bora za kibiashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki ifikapo mwaka 2025 na kwamba kampuni hiyo itaendelea kujiimarisha katika uwekezaji wa bidhaa ambazo ni rafiki kwa mazingira.

Daikin ni kampuni kutoka Japan ambayo inaongoza katika kuzalisha viyoyozi ambavyo ni rafiki kwa mazingira na ambayo ina kampuni tanzu inayozalisha bidhaa za namna hiyo nchini India.

# Naibu Spika awapa somo la kodi wajumbe Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amesema wajumbe wa baraza hilo wana jukumu kubwa la kuwa kiunganishi muhimu baina ya serikali na wananchi wao ikiwa katika taaluma ya kodi.

Alitoa rai hiyo jana wakati akifungua mafunzo ya matumizi ya mifumo katika ukusanyaji wa kodi na mikakati ya kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari kwa wajumbe wa Umoja wa Wawakilishi Wanawake (UWAWAZA) na watendaji wa baraza hilo.

Alisema wananchi wanapaswa kufahamu mambo muhimu kuhusu kodi na ufahamu ambao utajenga hamasa ya kufahamu wajibu wao katika masuala ya kodi.

"Pamoja na jukumu letu la kusimamia maendeleo ya wananchi katika majimbo, tuna wajibu pia wa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) katika kutoa taaluma ya kodi na ukusanyaji wa mapato kwa ujumla," alisema.

Pia alisema suala la ukusanyaji wa mapato ni jukumu la ZRA, lakini jukumu la kuhamasisha ulipwaji wa kodi ya serikali ni jukumu lao wajumbe hao ili wananchi wawajibike kwa mujibu wa sheria.

Mgeni aliwataka wajumbe hao kuwaelimisha wafanyabiashara wajisajili katika taasisi za kodi lakini pia watoe risiti za kielektroniki na kulipa kodi kwa usahihi na kwa wakati.

"Tuna wajibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kodi na tunaweza kufanya hivyo kwa kuwaonyesha matumizi halisi ya fedha za kodi walizolipa kupitia miradi ya maendeleo iliyomo katika jamii," alisema.

Aidha, alisema hiyo itawasaidia kujenga imani kwa mamlaka na serikali kwa sababu wataona matunda halisi ya kodi wanayoilipa.

Hivyo, aliwataka wajumbe hao kuwa mfano wa kudai risiti za kielektroniki kila wanapofanya manunuzi, kuwasisitiza wananchi kufanya hivyo kila wanapofanya manunuzi.

Alisema kwa kufanya hivyo kutawezesha kuwahudumia vyema wananchi kutokana na mapato yatakayokusanywa na serikali. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, ambaye ni Mwenyekiti wa UWAWAZA, alisema serikali inapoleta maendeleo kwa wananchi kutoka na fedha za kodi zinazokusanywa ni vyema kushirikiana katika kuwaelimisha.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa ZRA, Prof. Hemed Rashid Hikman, alisema ZRA, Baraza la Wawakilishi, Wizara ya Fedha na Mipango, walipakodi na wananchi ndiyo makundi yenye ulazima wa kujenga mahusiano ya karibu na kuelewana katika kusimamia kodi nchini.

Prof. Hikman alisema Baraza la Wawakilishi ndiyo wahusika wakuu wa masuala ya kodi, hivyo ni lazima kushirikiana pamoja na ZRA kufikia mikakati ya kuimarisha makusanyo ya kodi. "Ulimwengu wa sasa ni wa kidijitali katika kutumia mifumo ya TEHAMA ambayo itarahisisha upatikanaji wa kodi nchini hasa katika bandari, hoteli na uwanja wa ndege ili kuwa na mifumo ya pamoja ambayo itarahisisha kupatikana kwa mapato kwa urahisi," alisema Prof. Hikman.

Kamishna Mkuu wa ZRA, Yussuph Juma Mwenda, alisema ZRA imeweka mikakati mbalimbali kufikia ulipaji wa kodi wa hiari ikiwamo kuweka kambi za utoaji wa elimu, matumizi ya mifumo, kuteua mabalozi wa kodi, kufanya ukaguzi kwa walipakodi na kuhamasisha utoaji wa risiti.

Alisema masuala hayo yatasaidia kufikia malengo ya serikali ya kupata mapato yake.

Mwenda alisema hadi kufikia Mei mwaka huu ZRA imekusanya Sh. bilioni 528.6 ambao ni ufanisi wa asilimia 97.64 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 187.424 ambayo ni asilimia 54.97 kutoka Sh. bilioni 3.4.

Pia alibainisha kuwa kwa mwaka 2023/2024 ZRA imekadiria kukusanya Sh. bilioni 675 kutoka Sh. bilioni 579 ambalo ni ongezeko la asilimia 17.

Wajumbe wa baraza hilo waliipongeza ZRA kwa kuwapatia mafunzo hayo wakisema yatawasaidia katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kodi.




Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Prof. Hemed Rashid Hikman, akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye semina ya kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya kodi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampuni yawapiga msasa mawakala kuhusu teknolojia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya LG imeahidi kuendelea kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo mawakala wake ili waendane na teknolojia ya kisasa inayotumiwa na kampuni hiyo katika utengenezaji wa bidhaa zake.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa LG, Kanda ya Afrika Mashariki, Donglon Lee (pichai) wakati wa semina maalumu kwa mawakala wa LG.

"Tunathamini sana juhudi kubwa mnazaofanya nyinyi viongozi kwa michango yenu mbalimbali na ushirikiano mnaotoa ambao unawezesha kuainisha fursa za kiuchumi na hivyo kuchangia maboresho ya kiuchumi katika nchi hii nzuri," alisema.

Alisema kampuni hiyo inathamini umuhimu wa ushirikiano kwa njia ya kubadilishana uzoefu na elimu kwa lengo la kukuza huduma kwa wateja.

Lee alisema semina hiyo ni jukwaa ambalo litawawezesha kuimarisha mahusiano yetu na pia kufungua njia ya kukuza huduma kwa wateja na kuimarisha mahusiano kati ya LG na mawakala wake. "Lengo letu siyo tu kuimarisha ubora na uendelevu wa bidhaa zetu nchini Tanzania bali pia kuchangia katika mustakabali mwema katika kuboresha mazingira, afya za watu na ufanisi kwa ujumla katika kutoa huduma zetu katika nchi hii nzuri.

"Haya yote tunatarajia kuyafikia kupitia mahusiano na masuluhisho yanayoendelea kutolewa katika sekta mbalimbali katika nyanja kadhaa za huduma zikiwamo ukarimu, biashara za rejareja, elimu za kibiashara, huduma za afya na elimu kuhusiana na maswala ya usafiri," alisema.

Alisema LG inajivunia kitengo chake cha maonyesho ambacho kitawawezesha kutoa nyongeza ya thamani kubwa kwa wateja mnaowahudumia.



"Hiki ni kitengo maalum ambacho kinashughulikia bidhaa kama vile skrini za kidijitali, OLED, miundombinu za kuonyeshea sinema kwa njia za video kwa ujumla wake ikiwamo kwenye mahoteli ukanda mzima wa eneo hili la Afrika Mashariki," alisema.

Semina hiyo ilihudhuriwa na wadau mbalimbali ikiwamo mabalozi kutoka nchi ya Korea na India.

# Mambo sita chanzo ukatili kwa watoto

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia limebainisha mambo sita yanayosababisha unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwa watoto kama vitendo vya ulawiti na usagaji, ambavyo vinaingia pia shuleni, chanzo chake ni kushuka kwa ubora wa malezi yanayotolewa na wazazi.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto Afrika, Ofisa kutoka kitengo cha Dawati la Jinsia katika Kituo cha Polisi Tabata, Rajabu Ally, alisema kushuka kwa ubora wa malezi kumesababisha watoto wengi kukosa uangalizi, kutokuwa bora shuleni na katika nyanja tofauti.

Hafla ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika iliratibiwa na Umoja wa Wanawake wa Kutetea Haki za Watoto Tabata (WOMEN TAPO) wakishirikiana na Women Fund Tanzania Trust, ili kuendelea kutoa elimu na kupinga vitendo vya ukatili kwa watoto.

"Niko hapa kuwakumbusha wazazi wito wa Jeshi la Polisi kitengo cha Jinsia na Watoto, mzazi tunaomba uchukue jukumu la malezi ya kumtazama mtoto wako hakuna mtu ambaye anaweza akamtazama mtoto ambaye umekaa naye tumboni miezi tisa, akambadilisha kwa siku moja," alisema na kuongeza;

"Hakuna mtu ambaye anaweza kumbadilisha mtoto ambaye umekaa naye kwa muda wa miaka 17 akambadilisha kwa siku moja, zaidi itakuwa ni kesi na mtoto wako atafungwa, hivyo ili kuepuka hili tuzingatie malezi ya watoto wetu ili tujenge taifa la baadaye lililo bora," alisisitiza Rajabu.

Alisema jambo la pili ni makuzi, akieleza kuwa watoto wengi wazazi wamesahau kuangalia marafiki wa watoto, kuangalia watu anaocheza nao kuwa ni sahihi na kumpeleka katika njia sahihi, huku akibainisha kwamba kesi nyingi za watoto chanzo chake ni wanaocheza nao.

Aliwaomba wazazi kuangalia aina ya shule wanazowapeleka watoto na kujiuliza itawapatia kitu gani na katika kipindi cha likizo wafuatilie kuwa shule husika zinamjenga mtoto kimaadili na kumfanya atimize malengo yake.

Kadhalika, mahusiano aliyokuwa nayo mzazi na watu wengine, akisisitiza kuwa mtoto wa mwenzio ni wa kwako na kuna watu wameamua watoto wao wawe wa kwao kwa kuwafungia ndani hata kipindi cha likizo na hata kuwaletea walimu nyumbani, jambo linaloweza kusababisha mtoto kufanyiwa ukatili bila yeye kujua.

"Unaaminije kwamba huyu mtu uliyemleta nyumbani ni salama kwa mtoto. Kwenye suala la malezi hatutakiwi kumuamini mtu yeyote, hata mimi usiniamini kwasababu nina upungufu wangu lakini ninapokuwa katika kutimiza majukumu yangu niamini nieleze kinachokusibu ili nikusaidie," alisema Afande Rajabu.

Alitaja jambo la tano kuwa ni ndoa akibainisha kuwa sasa kuachana imekuwa ni fasheni, "mtu anaolewa leo anaachika kesho, huyu mtu alimchunguza huyu mwenza wake kabla ya kuoana naye? Unapokutana na mtu usitangulize vitu chunguza kwanza huyo mtu ana nia ya dhati na wewe."

"Angalia ni mtu sahihi atakwenda kuwa Mama au Baba bora wa familia au unakwenda kuweka rehani utu na maisha ya watoto wako, matusi na vipigo vinavyotokea kwenye ndoa vinasababishwa na chaguzi mbovu tunazofanya sisi wazazi, na mwisho wa siku tunaanza kusema mimba za bahati mbaya na hapo ndipo baadaye tunakuja kupata watoto ambao hawana uangalizi," alisema Rajabu.

"Taasisi mbalimbali kama TAPO wanatoa elimu na tunashirikiana nao ni mwaka wa tatu sasa, lakini watoto ni hao hao na idadi inazidi kuongezeka, maana yake ni kwamba uangalizi mbaya na kuvunjika kwa ndoa rate (kiwango) yake ni kubwa," alisema Rajabu.

Jambo la sita alisema kuwa ni historia ya maisha ya mzazi, akisisitiza wasiruhusu zikaenda kuharibu maisha ya watoto wao.

"Hakikisha ile historia yako mbaya ikawe ni funzo kwa mtoto, mueleze mtoto mapenzi katika umri mdogo yatakuponza angalia tofauti yangu na wewe kwenye umri nilikupata nikiwa na miaka 16 leo una 16 mimi nina 32, na wewe ukiingia huko nitapata mjukuu nikiwa na miaka 33, hatutamani kuona hayo mambo yanatokea," alisisitiza Afande Rajabu.

Aidha, alitoa wito kwa wazazi kuwahi kurudi nyumbani wakati watoto wakiwa likizo ili iwaongezee muda wa kufuatilia mienendo ya watoto wao kitaaluma na maadili.

Naye mwakilishi kutoka WOMEN TAPO, Stella Mbaga, alisema mtandao wao utaendelea kutoa elimu kwa kinamama na watoto ili watambue wajibu wao, akibainisha kuwa changamoto za kijinsia ni nyingi na kuwasisitiza wazazi kuwa makini na watoto wao ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia.



Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Mohamed Shekhe (katikati) na washiriki waliohitimu mafunzo ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa mazao ya samaki juu ya usalama, ubora na taratibu za ukaguzi kutoka Somali land. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# FETA yatakiwa kutanua wigo mafunzo ya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), umetakiwa kuongeza wigo wa ushirikiano kutoa elimu ya uvuvi.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Mohamed Shekh, alisema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku 30 ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa mazao ya samaki juu ya usalama, ubora na taratibu za ukaguzi kutoka nchini Somali land, yaliyofanyika Chuo cha Mafunzo ya Uvuvi, Kampasi ya Mbegani, Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Prof. Shekh alisema kuwa FETA inatakiwa kuongeza wigo wa ushirikiano na nchi mbalimbali kwa kuwa kuna rasilimali nyingi na wataalamu wapo wajitokeze na kutoa mafunzo ili kuongeza utaalam kwenye utekelezaji wa shughuli za uvuvi.

Vilevile, amewasihi kuendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kuendesha mafunzo hayo kwa watu wa ndani na nje ya nchi hasa wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi.

Wataalamu wa uvuvi kutoka Somali land hushiriki mafunzo hayo nchini ili kuongeza uwezo wa kusimamia rasilimali za uvuvi na kuhakikisha kuwa kuna kuwa na uvuvi endelevu nchini kwao.

Prof. Shekh alisema upo umuhimu mkubwa wa kuhakikisha mazao ya bahari yanakuwa na ubora na kuitaka FETA kuendelea kuhamasisha na kutoa mafunzo hayo kwa washiriki kutoka nchi mbalimbali.

Vilevile, amelishukuru Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), kwa kuwezesha kufanyika kwa mafunzo hayo na kuyaomba mashirika mengine kuiga mfano huo ili kuwafikia washiriki wengi zaidi.

Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Dk. Semvua Mzighani, alisema mafunzo yanayotolewa chuoni hapo msisitizo mkubwa huwa ni kwenye mafunzo kwa vitendo na matarajio yake watakaporejea nchini kwao watakwenda kutekeleza waliyofundishwa kwa vitendo na kuwaongezea ujuzi zaidi na kusaidia kutoa elimu kwa wengine.

Vyuo vyao vinatoa mafunzo ya uhandisi katika maji, ubora wa samaki, uvuvi na ubaharia, ukuzaji viumbe maji, mazingira na rasilimali za bahari, sayansi ya bahari na menejimenti ya bahari.

Akiongea kwa niaba ya wanafunzi wengine, rais wa wanafunzi hao kutoka Chuo cha Uvuvi nchini Somalia, Elm Mohamed, alisema ni vyema nchi hizo mbili zikashirikiana katika rasilimali zao kwa kuwa zinafanana hasa ukanda wa bahari pamoja na ufugaji.

Vilevile alishauri kushirikiana katika nyanja za utamaduni kwa kuwa utamaduni wa Watanzania ni mzuri.

## Wazee Muheza walalamika kukosa huduma ya matibabu

**Na Steven William,** MUHEZA

WAZEE wilayani Muheza wamelalamika kushindwa kuhudumiwa matibabu na kubaki wakipata shida wanapougua.

Malalamiko hayo waliyatoa katika kikao chao na Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Muheza, Jumaa Mhina, wakati akijitambulisha kwa wazee hao.

Diwani mstaafu wa CCM, Kata ya Mkuzi wilayani Muheza, Zuberi Semtauwa, alidai kuwa serikali imeshindwa kuwahudumia wazee matibabu na suala hilo kubaki propaganda.

Alisema kuwa wazee wanapofika hospitali ya teule wilayani hapo wanaambiwa wakanunue dawa na kuhoji fedha watapata wapi.

Semtauwa alisema kuwa wazee hao wana vitambulisho vinavyoonyesha kusamehewa na serikali kupata matibabu bure, lakini wanapofika hospitalini wanaambiwa vitambulisho hivyo vimepitwa na wakati.

Pia alisema Wilaya ya Muheza serikali imejenga hospitali ya wilaya eneo la Kijiji cha Lusanga, lakini mpaka sasa hakuna matibabu ya kutosha na majengo yake wanaishi ndege.

Katika hatua nyingine wazee hao waliomba Wilaya ya Muheza kuanzishwa halmashauri ya mji mdogo kama Korogwe ili wazidi kupiga hatua katika maendeleo.

Walisema, wazee wengi wamestaafu katika Halmashauri ya Muheza, lakini mpaka sasa hawajalipwa haki zao za kusafirisha mizigo kurudi kwao na michango ya NSSF hawajalipwa mpaka sasa kwa kuwa mwajiri alikuwa hapeleki michango.

## ‘Uelewa umuhimu wa bima mdogo nchini’

**Na Beatrice Shayo**

MENEJA wa Maendeleo wa Huduma za Bima ya Jubilee Allianz General Insurance, ameishauri serikali kuangalia uwezekano wa kusaidia uelewa katika masuala ya bima kwa walaji nchini ili wazitumie.

Hussen Nasoro alishauri hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu zawadi mbalimbali zilizowekwa kwa ajili ya wakala wao ili kuongeza ushindani.

Alisema bado watu wengi hawana uelewa katika masuala ya bima nchini, hivyo ni muhimu jitihada kuongezwa na serikali.

Alisema jitihida hizo zitasaidia wananchi kunufaika pindi wanapopata majanga mbalimbali yakiwamo ya moto badala ya kuishia kulalamika na huku uchumi wao ukiteketea.

Nasoro alisema bima za kilimo ni mpya, hivyo kuna haja kutolewa elimu ili wananchi wazielewe na kuzitumia kwa faida yao.

Alisema wanajitahidi kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa na kuwawekea bidhaa mbalimbali za bima ambazo zitakuwa nzuri na rahisi kwa walaji.

“Tulikuwa na bidhaa mpya, tumejitahidi kuwapa uelewa mawakala wetu waweze kwenda kuziuza, tumekuja na dukani tukiwa na ‘package insurance’ kwa ajili ya watu wenye maduka,” alisema.

Mkuu wa Wakala wa Bima ya Jubilee Allianz Insurance, Mary Kyuki, alisema kuna watu wengi wanapopata ajali katika masoko wanalia ikiwamo tukio la moto Soko la Kariakoo.

Alisema kuna bima kwa ajili ya wafanyabiashara ambayo gharama yake ni nafuu, hivyo itawasaidia kulipwa pindi wanapopata matatizo hayo.

“Ipo bima chee kabisa kwa ajili ya wafanyabiashara wetu wa Kariakoo na wenye masoko ya kawaida ili wanapopata majanga ya moto wawe na sehemu ya kukimbilia, wasiishie kulia na kulalamika. Bima zipo kwa ajili yao,” alisema.

**Tulikuwa na bidhaa mpya, tumejitahidi kuwapa uelewa mawakala wetu waweze kwenda kuziuza, tumekuja na dukani tukiwa na ‘package insurance’ kwa ajili ya watu wenye maduka.**

# Mkenda aitaka TET kutambua walimu wanaomudu ufundishaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), kuweka mazingira endelevu ya kutambua walimu wanaomudu vizuri stadi za ufundishaji kwenye shule za umma na binafsi.

Waziri Mkenda alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji Tuzo za Stadi za Ufundishaji kwa Walimu wa Elimu ya Awali na Msingi, na kueleza kuwa walimu wanahitaji motisha mbalimbali ikiwamo kutambua umuhimu wa kazi wanaofanya,

Alisema ubora wa elimu nchini pamoja na mageuzi ya elimu, bila kuwa na walimu wenye hamasa itakuwa ni kazi bure.



“Ningependa kwenye hili la kutambua stadi za ufundishaji. TET muweke mazingira endelevu, ninajua kwa sasa Mradi wa BOOST umewezesha na mmefika katika halmashauri 26. Ninataka mwende katika halmashauri zote na tuzo hizi ziwe endelevu na kazi hii mfanye pamoja na wizara ili hata baada ya mradi iweze kuendelea,”aliagiza Prof. Mkenda.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa walimu. Sera mpya ya elimu itaendeleza mafunzo kazini kwa walimu na itasisitiza fursa za walimu kusoma.

Waziri Mkenda alitumia fursa hiyo kuishukuri Benki ya Dunia (WB) kwa namna inavyofadhili miradi mbalimbali ya elimu nchini na pia kwa kuwezesha hafla ya utoaji wa tuzo kwa washindi wa stadi za ufundishaji kwa walimu wa elimu ya awali na msingi kupitia Mradi wa BOOST.

Mkurugenzi Mkazi wa WB Tanzania, Preeti Arora, alisema ushindani wa ujuzi wa kufundisha ni moja ya njia bora za maendeleo ya kitaaluma ya mwalimu.

“Kwa kushiriki katika ushindani, walimu wanahamasishwa kuendelea kuboresha mbinu zao za kufundisha, kupanua maarifa yao na kuendeleza mikakati mipya ya kushiriki na kuhamasisha wanafunzi wao kujifunza.

“Hii inasababisha ukuaji wao wa kitaaluma na huongeza ubora wa jumla wa elimu, hongera walimu wote mlioshinda,” alisema mkurugenzi huyo.

Mkurugenzi wa TET, Dk. Aneth Komba, alisema utoaji wa tuzo hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na WB, ukilenga kuboresha uwezo wa walimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi kupitia Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA).

“Shindano la Stadi za Ufundishaji kwa Walimu wa Elimu ya Awali na Msingi lilianza mwezi Aprili kwa kukusanya na kutathmini video za walimu zenye maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji wa kuhesabu pamoja na somo la Hisabati katika halmashauri 26 zinazotekeleza mradi wa BOOST,” alisema Dk. Komba.

Alisema pamoja na washindi kupata fedha, cheti na wengine ngao, video zao zitarekodiwa upya katika studio za TET na kupakiwa katika mfumo wa ujifunzaji na ufundishaji wa LMS na hivyo kuzidi kuleta chachu ya ufundishaji unaozingatia ujenzi wa umahiri.



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu (kulia), akiendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa ofisi ya chama hicho Jimbo la Kasulu Vijijini mkoani Kigoma juzi, ambapo zilipatikana Sh. milioni 1.2. **NA MPIGAPICHA WETU**

# RC, polisi wamwokoa mwanafunzi kwenye ndoa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akiwa na wadau wa msaada wa kisheria pamoja na Jeshi la Polisi mkoani humo, wamefanikiwa kutibua ndoa ya mwanafunzi wa kidato cha tano, mkazi wa Mwawaza Manispaa ya Shinyanga na Issa Mussa (21).

Tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 11 jioni nyumbani kwa mwanafunzi huyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Msaada wa Kisheria Mkoa wa Shinyanga, John Shija, alisema wakiwa katika utoaji wa elimu ya msaada wa kisheria walipata taarifa za siri kuwapo kwa ndoa hiyo iliyolenga kukatisha ndoto za mtoto huyo wa kike.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo waliweka mtego na kuwasiliana na polisi, pamoja na Mkuu wa Mkoa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, ambao walivamia harusi hiyo na kuwakamata wahusika huku wazazi wao wakikimbia.

“Taarifa tulizozipata mtoto huyu amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano huko Urambo mkoani Tabora, lakini wazazi wake hawakutaka aendelee na masomo yake, walitaka wamwozeshe ili wapate mali,” alisema Shija.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema hayupo tayari kuona watoto wa kike wanashindwa kufikia ndoto zao kwa tamaa ya wazazi kutaka kupata mali.

“Wazazi acheni watoto wenu wasome na kutimiza ndoto zao msiwe na tamaa ya kuwaozesha katika umri mdogo, na huyu mwanamme kama anampenda amsubiri hadi amalize Chuo Kikuu siyo sasa,” alisema Mndeme.

Aidha, aliagiza wazazi wa binti huyo ambao wamekimbia kusikojulikana, hadi Jumatatu (leo), wawe wamejisalimisha wenyewe polisi, kabla ya serikali kuwasaka.

Katika hatua nyingine alisema, serikali mkoani humo itasimama na binti huyo kuhakikisha anapata haki ya msingi ya kupata elimu ili aweze kufikia ndoto zake na akiwaonya wazazi wenye tamaa ya mali kupitia mabinti zao waache kwa kuwa mkono wa sheria unaangaza muda wote.

HABARI MICHEZO

# KOCHA SIMBA KUTUA COASTAL

Na Adam Fungamwango

KOCHA wa zamani wa Simba, Goran Kopunovic raia wa Serbia, yupo kwenye mzungumzo na klabu ya Coastal Union kwa ajili ya kuchukua mikoba ya kuifundisha timu hiyo.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa mbali na Kopunovic, pia Javi Martinez raia wa Mexico ni miongoni mwa makocha wanaopewa nafasi kubwa ya kuifundisha timu hiyo msimu ujao.**

Chanzo pia kimesema kuelekea msimu ujao klabu hiyo itapunguza gharama za uendeshaji kwa kutosajili wachezaji wengi wa kimataifa kama ilivyokuwa msimu uliomalizika.

"Tunaendelea na vikao, tunataka kuimarisha benchi letu la ufundi kwa ajili ya msimu ujao, tunataka kuwa na kocha wa kigeni na hadi sasa tuna majina mawili Goran na Javi tunajadiliana kuona nani anatufaa ingawa mpaka sasa Goran ana nafasi kubwa ya kuwa kocha wetu, anajua mazingira ya Tanzania," alisema mmoja wa viongozi wa klabu hiyo ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Aidha, alisema msimu ujao wanategemea kupunguza matumizi baada ya msimu uliopita kutumia zaidi ya Shilingi milioni 300 kwa ajili ya usajili wa wachezaji kutoka nje ya nchi na gharama ya vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini.

"Sasa tumeona tubaki na wachache tu, huenda msimu ujao tukawa na wanne tu, watano waliobaki tutawavunjia mikataba yao, lengo ni kuwa na wachezaji wazawa zaidi na kocha wa nje mwenye ujuzi zaidi," kilisema chanzo hicho.

Alisema licha ya kusaka kocha mpya, kocha wa sasa Fikirini Elias ataendelea kuwepo kikosini hapo na atahudumu kama kocha msaidizi.





Vijana wanaolelewa katika kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi kwenye uwanja huo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yakubu: Watanzania tufanye mazoezi kwa afya

Na Romana Mallya

KATIBU Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Said Yakubu, amewataka Watanzania kutenga muda wa kufanya mazoezi kila siku ili kuimarisha afya na kusisitiza anayefanya hivyo kwa muda wa saa moja, anaongeza maisha kwa saa tatu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Yoga iliyoandaliwa na Ubalozi wa India nchini yakiwa na kauli mbiu ya 'Yoga kwa Ulimwengu Mmoja ni Familia Moja,' alisema mazoezi yanaimarisha afya na kuongeza siku za kuishi duniani.

"Tujenge utamaduni wa kufanya mazoezi angalau kwa saa moja kila siku, wenzetu wa ubalozi wa India wanatukumbusha kupitia mazoezi haya ya Yoga," alisema Yakubu.

Maadhimisho hayo yanayofanyika kila mwaka yaliyohudhuriwa na watu zaidi ya 1,000 akiwamo mtoto mwenye umri wa miaka mitatu na mzee wa miaka 85.

Alisema mchezo wa Yoga unatambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na mazoezi yake yanahusisha vitu viwili, viungo vya mwili na fikra ambapo mtu anapata muda wa kufanya tafakuri kwa kukaa kimya peke yake na kuimarisha afya ya akili.

Alisema Yoga ni mazoezi kamili ambayo yanasaidia kuufanya mwili kuwa imara na kujiepusha na magonjwa mbalimbali yakiwamo yale yasiyoambukiza.

"Wito wangu kwa Watanzania watenge muda wao katika siku wa kufanya mazoezi kama haya. Nimesoma mahali ukifanya mazoezi kwa muda wa saa moja unaongeza maisha kwa saa tatu," alisema Yakubu.

Kwa upande wake, Balozi wa India Nchini Tanzania, Binaya Pradhan, alisema kwa mwaka huu wameamua kusherehekea siku hiyo kwa ukubwa kwa kuhusisha mikoa tisa ya Tanga, Dodoma, Mwanza, Arusha, Dodoma, Morogoro, Kilimanjaro, Zanzibar na Dar es Salaam yakihusisha diaspora wa India, Watanzania na wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa (UN).

Alisema siku ya Yoga hufanyika kila mwaka Juni 21, na lengo lake ni kutambua umuhimu wa mazoezi ambao husaidia kuimarisha afya ya akili.

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu ni ujumbe ambao wanataka kuupeleka duniani kuhusu umuhimu wa Yoga.

Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Zlatan Milisic, aliupongeza Ubalozi wa India Nchini Tanzania kwa kitendo cha kuandaa mazoezi hayo ambayo alisema huunganisha watu.

## Nassibu, Loren wajifua

Na Shufaa Lyimo

MABONDIA Nassibu Ramadhani na Loren Japhet wanaendelea na kambi kwa ajili ya kujiandaa na pambano lao ("PayBack Night ") ambalo linatarajiwa kufanyika Julai 15, mwaka huu kwenye uwanja wa Kinesi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Nassibu Ramadhani, alisema yupo kwenye maandalizi makubwa ya kuhakikisha anamtwanga mpinzani wake huyo.

"Nimejipanga vema kuelekea kwenye pambano hili ambalo litakuwa na ushindani mkubwa, ninaomba mashabiki wangu waje kwa wingi siku hiyo, nahidi sitowaangusha," alisema Nassibu.

Alisema amejiandaa kipindi kirefu kuhakikisha anawapa burudani mashabiki wake.

Aidha, kocha wa bondia huyo, Ibrahim Kombo, alisema hana wasiwasi na bondia wake kutokana na mazoezi anayoendelea kumpa.

"Ninaendelea kumnoa bondia wangu kuhakikisha anapata ushindi kwenye pambano hilo, sina hofu naye, ninavyomuona mazoezini ananipa uhakika wa kufanya vizuri kwenye pambano lake," alisema Kombo.

Kwa upande wake bondia Loren Kombo alisema ingawa mpinzani wake huyo ni mkongwe, hamuofii na ana uhakika wa kushinda pambano hilo.

## Wachezaji wakongwe Simba, Yanga waomba uwanja

Na Shufaa Lyimo

WACHEZAJI wa zamani wa klabu za Simba na Yanga wameiomba serikali iwaachie uwanja wa Gusepe uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam wautumie kwa ajili ya michezo badala ya mpango wa sasa wa kutaka kuuchukua kwa matumizi mengine.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Chamanzi Veterani, Ally Muhunzi, alisema wamesikitika kusikia serikali inataka kujenga shule eneo hilo ambalo liliwekwa maalum kwa ajili ya uwanja wa mazoezi.

"Huu uwanja ulikuwa umewekwa kwa ajili ya 'Day Care' lakini cha kushangaza diwani wetu anatuambia eneo hili linapaswa kujengwa shule jambo ambalo hatukubaliani nalo kwa kuwa huko wanapotaka kutupeleka pana umbali mrefu kutoka hapa, alisema Muhunzi.

Alisema watambua umuhimu wa elimu lakini wanaomba shule hiyo mpya ijengwe eneo lingine na kuwaachia uwanja huo kwa ajili ya michezo.

"Tunaiomba Serikali kutuachia eneo hili, michezo ni afya na inaleta umoja viongozi wetu tunawaomba sana," alisema Muhunzi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### YAMUULIZIA BARELLA

CHELSEA wamewauliza Inter Milan ikiwa watamjumuisha kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Barella, 26, katika makubaliano ya kubadilishana ambayo yatamfanya mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 30, kuhamia Italia kwa mkataba wa kudumu. ***(Corriere dello Sport)***

### PICKFORD AWANIWA MAN

KLABU ya Manchester United inatayarisha dau la pauni milioni 45 kwa mlinda mlango wa Everton, Jordan Pickford, 29. ***(Star Sunday)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imemwongeza beki wa kushoto wa Chelsea, Marc Cucurella, 24, kwenye orodha ya walengwa inayotaka kuwasajili msimu wa joto. ***(Sunday Mirror)***

### CHELSEA KUUZA NYOTA

CHELSEA pia inatazamia kumuuza mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 33, winga wa Morocco, Hakim Ziyech mwenye miaka 30, na golikipa wa Senegal, Edouard Mendy, 31, kwa klabu za Saudia. ***(Mundo Deportivo)***

### KUPELEKWA BRIGHTON

CHELSEA huenda ikamkabidhi kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 23, kwa Brighton kama sehemu ya makubaliano ya kumsajili kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo, 21. ***(Observer)***

### VIEGA AULIZIWA

LIVERPOOL na Chelsea zimeulizia kuhusu kiungo wa kati wa Celta Vigo na Hispania, Gabri Veiga, 21. ***(Fabrizio Romano)***

### KOULIBALY HUYO ARABUNI

KLABU ya Al-Hilal imefikia makubaliano ya maslahi binafsi na mlinzi wa Senegal, Kalidou Koulibaly, 31, juu ya uwezekano wa kuhama kutoka Chelsea. ***(Ekrem Konur)***

### ARTETA ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imezungumza na kocha wa Arsenal, Mikel Arteta kuhusu kuwa kocha wao mpya, huku mazungumzo yakiwa yamevunjika na kocha wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann. ***(RMC Sport)***

### RAYA SAFI SPURS

GOLIKIPA wa Brentford ya Hispania, David Raya, 27, amekubaliana maslahi binafsi na Tottenham Hotspur. ***(Fabrizio Romano)***

### GRAVENBERCH AVUTIA LIVER

KLABU ya Liverpool inavutiwa na kiungo wa kati wa Uholanzi, Ryan Gravenberch, 21, ambaye ameeleza kutoridhika kwake na kukosa muda wa kucheza kule Bayern Munich msimu uliopita. ***(Bild)***

### BRANTHWAITE ATAKIWA

WEST Ham imeanzisha uchunguzi kuhusu uwezekano wa kumpata beki wa Everton mwenye umri wa miaka 20, Jarrad Branthwaite ***(Football Insider)***

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# 'REAL MADRID ITAKUWA DHAIFU BILA BENZEMA'

**BARCELONA,** Hispania

●●● Ameondoka Real Madrid akiwa mfungaji bora wa pili wa muda wote wa klabu hiyo...

WINGA wa Barcelona, Ousmane Dembele, anaamini kuwa wapinzani wao Real Madrid watakuwa dhaifu baada ya kuondoka ghafla kwa Karim Benzema.

**Mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or kwa muda mrefu alitarajiwa kusaini mkataba mpya Santiago Bernabeu, lakini akabadili mawazo yake na kukamilisha uhamisho mzuri wa kwenda kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, Al Ittihad badala yake.**

Baada ya Cristiano Ronaldo kuondoka kwenda Juventus mnamo 2018, Benzema aliifunga Los Blancos hao mabao muhimu na kuiwezesha kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ameondoka Real Madrid akiwa mfungaji bora wa pili wa muda wote wa klabu hiyo akiwa amefunga mabao 354, idadi ambayo amezidiwa na Ronaldo pekee ambaye aliyefunga mabao 450.

Katika mahojiano na gazeti la Marca, Dembele alimzungumzia raia mwenzake huyo wa Ufaransa akisisitiza kuwa Real Madrid watapata tabu kutokana na kuondoka kwa mshambuliaji huyo.

"Bila Benzema, Real Madrid inapoteza sana kwa sababu yeye ndiye anayeshikilia Ballon d'Or na mchezaji mkubwa. Real Madrid bila Benzema sio sawa. Itakuwa hasara muhimu sana," alisema Dembele.

"Pia itakuwa hasara kubwa kwa LaLiga, kwa sababu ni mwanasoka anayefunga mabao mengi na kutoa asisti. Ni mchezaji wa aina yake."

Benzema alishindwa kutwaa tuzo ya mfungaji bora msimu huu, Pichichi Trophy ya LaLiga, iiyochukuliwa na mshambuliaji wa Barcelona, Robert Lewandowski.

Dembele alipoulizwa kuhusu uhusiano wake na mshambuliaji huyo wa Poland, ambaye aliwasili tu Barcelona majira ya joto yaliyopita akitokea Bayern Munich alijibu:

"Ni mchezaji mzuri, anafunga mabao mengi. Tayari tulifahamu hilo kutokana na kiwango chake akiwa Bayern. Nina uhusiano mzuri naye, ndani na nje ya uwanja. Ni mtu mzuri na mchezaji wa aina yake," alisema Dembele.



# RAIS WA BAYERN AKERWA NA XAVI

**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa Bayern Munich, Herbert Hainer, amemkosoa kocha mkuu wa Barcelona, Xavi kwa kukiri nia yake ya kutaka kumsajili kiungo, Joshua Kimmich.

Ingawa Bayern wamedhamiria kuendelea kumshikilia Kimmich, 90minutes inaelewa kuwa wawakilishi wa Mjerumani huyo wamezungumza na klabu kadhaa kubwa za Ulaya ikiwa ni pamoja na Barcelona.

Xavi aliulizwa kuhusu nia ya timu yake kwa Kimmich mwezi uliopita na hakusita kuzungumzia nia yake ya kufanya kazi na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, na aliliambia gazeti la Mundo Deportivo: "Ni mchezaji wa kiwango cha juu, ambaye anaelewa mchezo kwa njia ya ajabu. Kama kutakuwa na mlango wazi, kutakuwa na mazungumzo na Bayern."

Maneno yake yanaonekana kumkatisha tamaa Hainer, ambaye alitilia shaka mwenendo wa Xavi katika mahojiano ya hivi majuzi na Sky Sports Ujerumani.

"Kwanza kabisa, Xavi alikuwa mchezaji bora na ninaiheshimu sana Barcelona," alisema Hainer.

Akithibitisha nia yake ya kutaka kumbakisha Kimmich, Haimer aliongeza: "Joshua ni kiongozi, ameshinda mataji mengi na sisi na pia ataendelea kushinda mataji na sisi katika siku zijazo. Yuko katika mipango yetu ya siku zijazo na mmoja wa wachezaji wetu muhimu."



# PSG, Nagelsmann washindwana

**PARIS,** Ufaransa

JULIAN Nagelsmann hatakuwa kocha wa Klabu ya Paris Saint-Germain msimu ujao baada ya mazungumzo kati ya pande hizo mbili kuvunjika, vyanzo viliiambia ESPN.

Mabingwa hao wa Ufaransa sasa wameondoa mawazo ya kuendelea na Nagelsmann, vyanzo vimeiambia ESPN, ikipunguza orodha yao fupi kwa wagombea wanne, Luis Enrique, Sergio Conceicao, Marcelo Gallardo na Thiago Motta.

Kocha wa Porto Conceicao amewasiliana na klabu hiyo, huku kocha wa zamani wa Barcelona na Hispania, Enrique akiungwa mkono na maofisa wa klabu hiyo kutoka Qatar.

PSG pia wanavutiwa na wachezaji wa zamani Gallardo, ambaye sasa anafundisha klabu ya River Plate ya Argentina, na Motta, ambaye anainoa Bologna ya Serie A.

Yeyote atakayechukua mikoba ya PSG ataingia wakati wa msukosuko katika klabu hiyo ambayo imeshuhudia Lionel Messi na Sergio Ramos wakiondoka, pamoja na Kylian Mbappe akithibitisha Jumatatu kwamba ana nia ya kuondoka kwa uhamisho wa bure msimu ujao wa joto.

ESPN iliripoti mwezi uliopita kwamba Neymar pia yuko tayari kuhama kutoka mji mkuu wa Ufaransa.

PSG ilinyanyua taji la Ligue 1 kwa mara ya 11 iliyovunja rekodi msimu huu, lakini kuondolewa kwenye hatua ya 16 bora kutoka kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya kulifanya kocha Christophe Galtier atimuliwe baada ya kuifundisha kwa msimu mmoja pekee.

# Southgate ambadilisha Alexander-Arnold

**LONDON,** Engand

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, amesema anapanga kumpa Trent Alexander-Arnold nafasi zaidi katika safu ya kiungo baada ya beki huyo wa kulia wa Liverpool kung'ara katika nafasi yake mpya ya kimataifa wakati wa ushindi wa 4-0 dhidi ya Malta Ijumaa katika mechi yao ya kufuzu Euro 2024.

Alexander-Arnold alistawi katika nafasi ya kiungo akiwa Liverpool katika miezi ya mwisho ya msimu wa 2022-23 na alikuwa katika ubunifu wake bora dhidi ya Malta katika mchezo wake wa kwanza wa kimataifa kwa mwaka huu, akifunga bao la mbali.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ametatizika kushikilia nafasi ya kuanzia chini ya Southgate na kupata mechi yake ya 19 pekee tangu acheze mechi yake ya kwanza mwaka 2018, huku kocha akimpendelea Reece James, Kyle Walker au Kieran Trippier katika nafasi ya beki wa pembeni.

Ilikuwa ni mara yake ya kwanza kucheza katika nafasi ya juu kwa England tangu alipotumiwa bila mafanikio dhidi ya Andorra mwaka wa 2021. Lakini baada ya maonyesho hayo mazuri siku ya Ijumaa, Southgate alisema anataka kutumia ubunifu wa Alexander-Arnold.

"Sina maswali kichwani anaweza kufanya hivyo," alisema Southgate.

"Tulizungumza kuhusu hilo wiki nne zilizopita kwenye simu na amefurahishwa na hilo. Alionyesha kile tunachofikiria anaweza kukiweza na anatupa kitu tofauti na viungo wetu wengine.

"Bila shaka, mengi yatakayotokea yatategemea klabu yake. Ukweli ni kwamba amekuwa akicheza kwa kiasi fulani ndani na mpira, ingawa ndani zaidi, umesaidia mabadiliko yake."

Alexander-Arnold alifurahia kucheza nafasi hiyo akiwa amevalia jezi namba 10, na akasema anatumaini itamsaidia zaidi kuwa na nafasi kwenye kikosi cha Southgate.

"Sijaicheza sana, lakini inahisi vizuri," alisema. "Najisikia kawaida. Ni mahali pengine ninaweza kujiona nikicheza. Nataka kuhakikisha kuwa mara kwa mara niko kwenye jedwali la timu, na huo ulikuwa msingi mzuri wa kujenga.



## Wachezaji Yanga wajibebesha deni msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga wamesema wana deni kubwa la msimu kurudia kile walichokifanya msimu huu au zaidi ili kuendelea kukonga nyoyo za wanachama na mashabiki wao.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam jana, wachezaji hao wamesema kufanya vizuri ni jambo moja, lakini kuendelea kufanya hivyo na zaidi ya hapo ni kazi kubwa, hivyo wanapokwenda mapumziko watahakikisha wanajipanga vyema ili msimu ujao waje na makali zaidi ya msimu huu.

Denis Nkane, winga wa timu hiyo alisema ulikuwa msimu mgumu kuliko yote ambayo amewahi kukutana nao kwenye maisha yake ya soka na hasa alipojiunga na Yanga.

Yanga imetwaa Ngao ya Jamii, Ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA, ikiwa ni pamoja na kufika fainali za Kombe la Shirikisho barani Afrika.

"Tumefurahi tumekuwa na msimu mzuri sana wa mafanikio, lakini ulikuwa ni msimu mgumu kuliko mingine yote niliyocheza, ligi imekuwa ngumu kutokana na uwekezaji mkubwa, klabu ilikuwa na malengo yake nayo yalikuwa ni lazima tutetee mataji yetu yote; ya ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA, na mimi mwenyewe kuna wakati nilipata majeraha na kushindwa kuitumikia, lakini nashukuru nikapona na kuanza kucheza tena, nadhani msimu ujao itabidi tukaze buti ili kuendelea kupambania makombe yetu," alisema mchezaji huyo aliyesajiliwa misimu miwili iliyopita akitokea Biashara United.

## Stars yafufua matumaini

INATOKA UKURASA 24

kulia, Najeeb alipopanda mbele na kupiga krosi iliyokuwa inasubiriwa kwa hamu na wachezaji wenzake, lakini kwa bahati mbaya, ukatoka juu kidogo la lango.

Kibu, aliyekuwa kwenye kiwango kizuri kwenye mechi ya jana na kumsumbua mno beki wa kulia Najeeb, alifanya kazi ya ziada alipowatoka mabeki wa Niger dakika ya 12, na kumpa pasi Dickson Job ambaye alimimina majaro iliyokuwa ikisubiriwa na Mbwana Samatta, lakini kabla haujatua kichwani kwake, mabeki wa Niger waliuwahi na kuutoa kona, huku Kocha Mkuu wa Stars akiwa ameshasimama kutaka kushangilia bao.

Dakika nne baadaye, Msuva alipata mpira kirahisi baada ya beki mmoja wa Niger kuanguka chini peke yake, akapiga krosi iliyounganishwa na Kibu, isivyo bahati, ukatoka kidogo tu pembeni ya lango la wapinzani.

Baada ya dakika 20 kupita, kasi ya Stars ilionekana kupungua na Niger kuanza kutawala pambano ikipiga pasi fupi fupi.

Moja kati ya shambulizi kali lililofanywa ni lile la dakika ya 38, wakati mshambuliaji tegemeo wa timu hiyo, Daniel Sosah alipowazidi maarifa mabeki Bakari Mwamnyeto na Ibrahim Abdallah 'Bacca' na hapo hapo, kipa Beno Kakolanya akiwa ametoka langoni.



# ADEBAYOR ANUKIA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa RS Berkane ya Morocco, Victorien Adebayor, amekubali kujiunga na klabu ya Simba kwa ajili ya msimu ujao wa ligi baada ya mazungumzo na viongozi wa klabu hiyo jijini Dar es Salaam.

**Adebayor, mwenye umri wa miaka 26, amekubali kujiunga na klabu hiyo, baada kushindikana kujiunga nayo msimu uliopita alipokuwa akiichezea klabu ya US Gendarmerie ya Niger.**

Taarifa kutoka ndani ya klabu ya Simba zinasema kuwa, viongozi wa klabu hiyo walifanya mazungumzo na mchezaji huyo na amekubali kusaini mkataba wa miaka miwili wenye chaguo la kuongeza mwingine mmoja baadaye.

"Tumezungumzia pia mshahara, bonasi na marupurupu mengine, kifupi asilimia 90 tayari mchezaji huyo atavaa jezi za Simba msimu ujao," kilisema chanzo kutoka ndani ya klabu ya Simba.

Adebayor alikuwa Tanzania na kikosi chake cha timu ya taifa ya Niger ambacho jana kilicheza mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zinazotarajiwa kufanyika mwakani nchini Ivory Coast.

Hata hivyo kwa sasa mchezaji huyo bado ana mkataba wa klabu ya RS Berkane, na Simba inatakiwa kuongea na klabu yake hiyo kwa ajili ya kumsajili kwani haitompata kama mchezaji huru.

Kwa sasa Adebayor amekuwa hana namba ya kudumu kwenye kikosi cha RS Berkane iliyomsajili mwishoni mwa mwaka jana akitokea US Gendarmerie.

Klabu hiyo iliipiku Simba kwenye kinyang'anyiro cha kumpata mchezaji huyo ambaye mwenyewe alionekana kuwa na mapenzi na Wekundu wa Msimbazi, lakini mwisho wa siku wakala wake akaamua kumlazimisha kwenda Morocco kutokana na ofa nzuri walioipata.

Simba ilimuona winga huyo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika hatua ya makundi mwanzoni mwa msimu uliopita na ilikuwa na nia ya kumsajili kwa ajili ya msimu uliomalizika wa mashindano lakini ilimkosa dakika za mwisho kabla ya dirisha la usajili halijafungwa.



Wachezaji wa Timu ya Taifa Stars wakishangilia baada ya kupata bao lililofungwa na Simon Msuva, katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za AFCON dhidi ya Niger uliochezwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mayele aomba kuondoka Yanga

INATOKA UKURASA 24

gumzo kwa ajili ya mikataba mipya.

"Mazungumzo yanaendelea, uongozi tumeamua kubaki na makocha hawa ambao watakuwa na msaada mkubwa na kocha mpya atakayeajiriwa hivi karibuni," alisema kiongozi huyo.

Alisema mbali na makocha hao, tayari mchakato wa kumpata kocha mkuu umeanza ambapo wamepokea zaidi ya maombi 100 ya makocha kuomba kazi ya kuifundisha timu hiyo.

"Kesho (leo) tutakaa na kupitia CV za makocha wote walioomba kazi, baada ya kujiridhisha tutamtangaza kocha wetu mpya atakayechukua nafasi ya Nabi (Nasreddine)," alisema.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema baada ya kutoa taarifa ya kuachana na Nabi, makocha wengi wametuma CV zao kutaka nafasi hiyo.

Alisema katika orodha ya makocha ambao wanaomba kazi hiyo, wapo makocha wakubwa ambao wanatamani kufanya kazi na Yanga.

"Binafsi sikutegemea kuona majina ya makocha wakubwa kama waliopo, baada ya kufanya vizuri katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC), Yanga imekuwa kubwa zaidi kila mmoja anatamani kufanya kazi katika klabu hii ya mafanikio, uongozi utapitia maombi yote na kuamua nani wa kumpa nafasi, mashabiki wasubiri tu," alisema Kamwe.

Aidha, alisema watampa kazi kocha mwenye mafanikio ya soka la Afrika hasa yule ambaye amefanikiwa kutwaa taji lolote la CAF.

# Michezo

Jumatatu Juni 19, 2023

Nipashe




Southgate ambadilisha Alexander-Arnold UKURASA 22



Nyota wa Timu ya Taifa 'Taifa Stars', Novatius Dismas (kulia), akimtoka mchezaji wa Niger, katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za AFCON uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, Stars ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAYELE AOMBA KUONDOKA YANGA

Na Saada Akida

## ●●● Viongozi wapambana kumbakisha, Kaizer Chief yatajwa...

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Fiston Mayele ameomba kuondoka kwenye kikosi hicho na kwenda kutafuta changamoto nyingine huku klabu ya Kaizer Chief ikatajwa kumtaka Mkongomani huyo.

**Taarifa ambayo Nipashe imeipata, nyota huyo ameonyesha dhamira ya kutoendelea kuitumikia klabu hiyo na anataka changamoto mpya.**

Mmoja wa viongozi wa Yanga aliiambia Nipashe kuwa kwa sasa wanapambana kuhakikisha wanaendelea kupata huduma ya nyota huyo aliyechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yao msimu huu.

"Viongozi wanapambana kuhakikisha Mayele anabaki, lakini mwenyewe ameomba kuondoka na ameuomba uongozi kukubali ofa yoyote itakayokuja kumuhusu yeye, kama viongozi tunatamani kuendelea kuwa na Mayele kikosini," alisema kiongozi huyo na kuongeza;

"Viongozi hatutakuwa na jinsi kama akibaki na msimamo wake kwa sababu tayari mchezaji ameshataka kuondoka huwezi kumzuia, lakini bado tunapambana kuhakikisha tunambakisha," alisema.

Aidha, alisema wapo wachezaji wengine ambao wameandika barua kuomba kuvunja mikataba yao ili waende wakatafute changamoto nyingine.

"Kuna wachezaji wengine wenyewe wameomba kuondoka, mazungumzo yanaendelea na mambo yatawekwa wazi siku si nyingi," alisema kiongozi huyo.



Wapambana kuwabakisha makocha

Katika hatua nyingine, uongozi wa Yanga upo kwenye mazungumzo ya kuwabakisha makocha wake wasaidizi Helmy Gueldich na Khalil Ben Youssef.

Makocha hao mikataba yao imemalizika baada ya kuisha kwa msimu huu wa 2022/2023, kwa sasa wapo kwenye mazun-

INAENDELEA UKURASA 23

# Stars yafufua matumaini kutinga AFCON

Na Adam Fungamwango

BAO pekee lililofungwa na mchezaji wa kimataifa wa Tanzania anayecheza soka la kulipwa kwenye klabu ya Al Qadsiah ya Saudi Arabia, Simon Msuva, jana liliifanya timu ya taifa, Taifa Stars kufufua matumaini ya kukata tiketi, kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajiwa kufanyika mwakani Ivory Coast kwa kuifunga Niger bao 1-0.

Winga huyo alipachika bao hilo dakika ya 69, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na kiungo Novatus Dismas, anayecheza soka la kulipwa Ubelgiji kwenye klabu ya Zulte Waregem.

Faulo iliyopigwa na Dickson Job winga ya kulia, ilikatisha hadi winga ya kushoto, kiungo huyo akauchukua mpira na kuwazidi nguvu na maarifa mabeki wa Niger kabla ya kupiga krosi iliyounganishwa na Msuva, akiiwezesha Tanzania kupata ushindi wa kwanza nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwenye mechi hiyo ya Kundi F, ya kusaka tiketi ya kucheza fainali hizo zinazotarajia kuanzia Januari 13 mwakani, hadi Februari 11, Stars ilitawala zaidi kipindi cha kwanza, hasa dakika 20 za mwanzo na Niger ilitawala kipindi cha pili hasa dakika 15 za mwisho.

Sekunde ya 30 tu, Kibu Denis alimtoka Najeeb Yakoub na kupiga krosi iliyowababatiza mabeki wa Niger na kuwa kona ambayo ilienda kupigwa na Mudathir Yahaya na kuunganishwa vema na Simon Msuva, lakini ukatoka kidogo nje ya lango.

Stars iliendelea kulisakama lango la wapinzani wao, dakika ya nne ya mchezo, Mudathir Yahaya, akiwa umbali wa mita zipatazo 35, aliachia kombora kali ambalo kipa Djibrilla Kassali Djibo alitaka kuudaka, lakini ukamtoka na kwa bahati nzuri akauwahi tena.

Niger ilijibu shambulizi dakika ya tano, wakati beki wa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >